




**Fidia** ya ajali lori mafuta Dar bado kitendawili

UKURASA 3



Nipashe

NANE NANE 2023

Jumanne Agosti 8, 2023

"VIJANA NA WANAWAKE NI MSINGI IMARA WA MFUMO ENDELEVU WA CHAKULA"

Ukurasa 12

TARI 'inavyomtoa' mkulima shambani, ikitekeleza agizo la Rais kunusuru ngano

AFRO WORLD AGRI FOOD 2023

Ukurasa 13

Baada ya kuwasherehekea wakulima sasa ni kongamano kimataifa la chakula

ELIMU

NA PETER ORWA

Ubunifu kilimo Awamu ya Sita katika staili kuendeleza yake Baba wa Taifa

WAKATI unapatikana uhuru wa nchi, moja ya mbinu mkakati wa maendeleo ililenga sekta ya kilimo, kuanzia kwenye falsafa ya umma, sera na mfumo wa uchumi kitaifa.

Ikirejewa maana ya maendeleo kupitia tafsiri ya kitafiti ya ya mwanazuoni Profesa Walter Rodney, mwenye historia ya kushika chaki, pia kuandika vitabu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anaitafsiri maendeleo kuwa ni mabadiliko ya kusonga kwenye idadi na ubora wa vitu vinayoandaliwa au kuzalishwa.

Katika mikakati yake kihistoria, mwasisi wa taifa Mwalimu Julius Nyerere, akaiweka sekta kilimo katika mikondo tofauti, ikiwamo kuzamisha elimu kwa wakulima.

Ikianzia na hotuba yake kihistoria, hadi matendo na hususani Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Nchi, 1964 - 1969 ambayo kimsingi ni dira ya taifa hadi sasa, kilimo kimeshika nafasi yake kitaifa ikiwa 'sekta mama' mkuu huyo wa nchi akiwajibika katika matamshi ya hotuba kila mara akisistiza 'mpunga (umbali) tunapanda nchi moja moja...'

Hata baadaye mwaka 1967, kwenye utekelezaji wa Azimio la Arusha, kupitia matamshi na maandiko yake mbalimbali kama vile nadharia ya 'Elimu ya Kujitegema' na maudhui ya vitabu kama cha Ujamaa, nafasi ya upeo katika kuwa na kilimo bora kwa mkulima ikashuhudiwa.

Elimu ya Kujitegemea, nadharia aliyohimzia zaidi Mwalimu Nyerere ililenga kumboresha msomi wa Kitanzania, kuanzia elimu ya msingi ambayo imebaki kuwa ya lazima, hata chini ya hapo kwa ambao hawakuipata, wakinufaishwa kwenye 'kisomo chenye manufaa.'

Inapoangaliwa kwa kina, mkulima amekuwa na nafasi kubwa ikizingatiwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wakati huo walikuwa wakulima na kwa maana hiyo. Hapo inamaanisha ni elimu kwa mkulima, kukidhi maisha yake nyumbani na ya shambani.

Hadi sasa Elimu ya Kujitegemea imebaki kuwa tawi kubwa ya elimu kitaifa, ikitiliwa maanani ni sehemu ya Sera ya Elimu ya sasa na kilimo kikiendelea kushika nafasi kubwa ya uchumi, huku serikali iliyoko madarakani chini ya Rais. Dk. Samia Suluhu Hassan, ikiweka mkakati kukifanya kuwa mwajiri mkuu kitaifa.

Kwa mujibu wa malengo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), wana mtazamo mkubwa katika kundi la kinamama na vijana, ambao ndio jeshi kubwa kitaifa.

Tayari Mwalimu Nyerere, tangu anaasisi uhuru wa nchi alishaweka mkazo kwa majukumu ya TARI, akizipanua na kuyapa malengo mapya, kukidhi mahitaji ya kitaifa, kutoka kwenye yale ya kikoloni.

Kwa upande wa ubunifu wa elimu ya juu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akakipatia tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo Morogoro (sasa SUA), ambacho hadi leo ni mbia mkubwa wa TARI.

AWAMU YA SITA

Kadri inavyoangaliwa mikakati, falsafa, sera, hadi malengo ya sekta za kilimo na mifugo nchini, daima inasimama katika mstari mmoja na ubunifu wa Mwalimu Nyerere, hasa kuanzia mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano nchini wa mwaka 1964 hadi 1969, iliyofuatiwa na nyingine kama hiyo.

Hadi sasa, Rais wa serikali ya Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kipaumbele kikubwa kwa sekta ya kilimo, katika falsafa na kipaumbele kilekile cha mwaka 1964, tofauti ikiwa ni mahitaji ya wakati husika.

Wakati mtazamo uliopita ulilenga kujitosheleza kwa chakula, pia kuepuka hali ya 'kuzalisha tusichokitumia na kutumia tusichozalisha' jibu lake ilikuwa ni kupanua mashamba kuzalisha chakula na malighafi, pia kuwa na viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi hayo; kinachofanyika nchini 'operesheni viwanda.'

Imeshuhudiwa juhudi binafsi za Rais Dk. Samia, pia kiserikali katika sura pana na mikakati akiwekeza nguvu kubuniwa viwanda, sasa kukionekana viwanda vipya vya sukari kumaliza uhaba huo, huku wakala wa kihistoria wa mageuzi ya teknolojia shambani TARI, ikipewa majukumu maalumu.

TARI inawajibika sasa kuhakikisha, ifikapo mwaka 2030, kuwezesha nchi ijitegemee kwa upa-

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua mazao ya kazi za shambani. Anayempa taarifa ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MTANDAO.**

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11


# Nipashe


Jumanne Agosti 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581396

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Ukumbi wafurika, hukumu kesi ya Bandari ikisogezwa

UKURASA 2

## YALIYOMO



UKURASA WA 3

### LHRC YATATUA MIGOGORO 1,500 YA MIRATHI MIEZI 6

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kimepokea jumla ya mashauri 1,531...

## Jopo madaktari bingwa mifupa Marekani laweka kambi nchini

UKURASA 5



Baadhi ya wananchi wakitoka nje ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya baada ya kesi ya mkataba ya DP World kuahirishwa hukumu yake jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


RIPOTI MAALUM

# Usafishaji kucha mitaani unavyobeba hatari kiafya

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YAIONYA AZAM NGAO YA JAMII** UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiagana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, baada ya mazungumzo Ikulu ya Zanzibar wiki iliyopita. Kushoto ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu aonya wizi wa mafuta magari ya serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekemea wizi wa mafuta kwa madereva wa magari ya serikali.

Vilevile, ameagiza ifikapo Oktoba 30 mwaka huu, taasisi zote zenye magari yaliyoegeshwa kwa muda mrefu, yawe yametengenezwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na kuondolewa katika karakana ya wakala huo.

Waziri Mkuu pia ameagiza magari yaliyotumika muda mrefu ambayo yamekuwa mzigo kwa serikali, maofisa masuhuli waangalie namna ya kuwakopesha au kuwauzia watumishi wanayoyahitaji kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo badala ya kuyaacha maegesho.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana jijini hapa wakati wa hafla ya kukabidhi magari 30 na vitendea kazi vya kupima afya na usalama mahali pa kazi kwa ofisi za mikoa za Idara ya Kazi na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Aliwataka maofisa masuhuli na vyombo vya usalama wahakikishe wanafanya ufuatiliaji kikamilifu na kuchukua hatua kwa watakaobainika [as printed: "hatua kuhusu taarifa za baadhi ya madereva kujihusisha na wizi wa mafuta kwa kudanganya taarifa za umbali au kuuza mafuta kupitia vituo vya mafuta au kutoka katika magari yao. Ni Vitendo vinavyokiuka masharti ya ajira na ni hujuma kwa serikali.

Alisema Maofisa Usafiri katika idara zote za serikali wanapaswa kuzingatia mpango maalum wa matengenezo ya magari kufanyika kwa wakati, kutumia vifaa vyenye ubora na kutunza taarifa za kila chombo.

"Hii itapunguza idadi ya magari yanayowekwa katika maegesho kwa muda mrefu ikiwamo katika karakana za TEMESA. Ifikapo tarehe 30 Oktoba, 2023, taasisi zote zenye magari yaliyoegeshwa kwa muda mrefu TEMESA, yawe yametengenezwa na kuondolewa na nipate taarifa," aliagiza.

Majaliwa pia aliwataka viongozi wapange vizuri ratiba za kazi na kuhakikisha madereva wanapata muda wa kupumzika na kulipwa kikamilifu stahiki zao.

"Nisisitize madereva wote wa serikali na taasisi zake, zingatieni sheria na taratibu za usalama barabarani na sheria za nchi.



"Nchi hii inaongozwa na utawala wa sheria, kuendesha gari la serikali haimaanishi mmepewa rungu la kuvunja sheria, bali mnapaswa kuwa mfano wa kuzingatia sheria za nchi kuhusu usalama barabarani," alionya.

Pamoja na hayo, Majaliwa pia aliwaagiza watumishi wa umma nchini wahakikishe kero za wananchi zilizoko katika maeneo yao zinatatuliwa ili wananchi wasilazimike kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa kwa masuala ambayo yangeweza kufanyiwa kazi kwa nafasi zao.

Majaliwa pia aliagiza kila idara iliyopokea magari hayo kuhakikisha yanatunzwa na kutumika kwa shughuli za umma na si za binafsi.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali ina mpango wa kuongeza magari mengine 28 ambapo kati ya hayo, magari manane ni kwa ajili ya idara ya kazi na 20 ya OSHA.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema magari na vitendea kazi hivyo vimegharimu Sh. bilioni 4.3 huku akiomba kuongezwa maofisa kazi ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Rais wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhoka, alisema wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu, waliiomba serikali kuziangalia taasisi zake, ikiwamo OSHA, kwa kuwapatia vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

# Ukumbi wa korti wafurika watu, uamuzi kesi DP World Alhamisi

**Na Kulwa Mzee,** MBEYA

UKUMBI wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya jana ulifurika wananchi waliofika kwa ajili ya kusikiliza uamuzi wa kupinga mkataba unaolenga kuendesha, kuwekeza na kuendeleza bandari nchini.

Wananchi wengi walifika katika viunga vya mahakama hiyo jana asubuhi na ilipofika saa mbili walianza kupanga mstari kwa ajili ya kuandikisha kuingia katika ukumbi wa wazi namba nne.

Ukumbi wa wazi ulijaa na watu wengine walilazimika kusimama. Mtumishi wa mahakama alitoa tangazo kwamba shauri hilo litasikilizwa katika kumbi mbili kutokana na wingi wa watu.

Ilitangazwa ukumbi wa pili wananchi watakuwa wakisikiliza uamuzi kupitia video.

Baada ya matangazo hayo yaliyotolewa saa tatu asubuhi, ilipotimu saa nne asubuhi, aliingia Msajili wa Mahakama hiyo kwa ajili ya shauri hilo.

Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo, akiwawakilisha Wajibu Maombi, aliifahamisha mahakama kuwa kwa upande wao walikuwa tayari kusikiliza uamuzi na maelekezo mengine yoyote ya mahakama.

Wakili wa Waleta Maombi, Mpale Mpoki, alidai kwa upande wao pia walikuwa tayari kupokea uamuzi.

Msajili wa Mahakama Kuu, Projest Kahyoza alisema mara ya mwisho baada ya pande zote mbili kukamilisha kuwasilisha hoja, mahakama ilipanga shauri lije jana kwa ajili ya uamuzi.

"Mwenyekiti wa Jopo Jaji Dunstan Ndunguru kapata dharura, jopo walikubaliana wasome uamuzi wakiwa pamoja kwa tarehe itakayopangwa, mwenyekiti atakuwapo. Shauri linaahirishwa hadi Agosti 10 mwaka huu saa tatu asubuhi," alisema Msajili Kahyoza.

Jopo la majaji katika shauri hilo linahusisha Jaji Ndunguru ambaye ni kiongozi wa jopo, Jaji Mustafa Ismail na Jaji Abdi Kagomba.

Shauri hilo lilifunguliwa na wanasheria watatu kutoka mikoa tofauti; Alphonce Lusako, Emmanuel Chengula, Raphael Ngonde na Mwananchi Frank Nyalus dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge la Tanzania, ambaye ni mtendaji mkuu na mratibu wa shughuli za Bunge.

Walalamikaji wanawakilishwa na Mawakili Mpale Mpoki, Boniface Mwabukusi, Livino Ngalimitumba na Philipo Mwakilima.

Pande zote mbili katika shauri hilo zilikubaliana hoja sita ndizo zinazobishaniwa mahakamani ikiwamo kama kutia saini, kuwasilisha bungeni na kuridhia mkataba wa Tanzania na Dubai kulikiuka kifungu cha 11(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Rasilimali na Maliasili, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2017 kikisomwa pamoja na Sheria ya Mapitio na Majadiliano ya Mikataba ya Masharti Hasi, Sheria Na. 6 ya Mwaka 2017.

Hoja ya pili ni kama umma uliarifiwa na kupewa muda mwafaka kushiriki na kutoa maoni yao kama sheria zinavyotaka kuhusiana na utaratibu wa kupitisha na kuridhia mikataba.

Katika shauri hilo, hoja ya tatu ni kama ibara ya 2, 4(2) zinakiuka Ibara namba 1,8. Hoja nyingine ni kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ni mkataba na hoja ya tano kama Ibara ya 2 na 23 ya IGA zinakiuka kifungu cha 25 cha Sheria za Mikataba Tanzania.

hoja ya sita inayobishaniwa ni kama IGA kati ya Tanzania na Dubai ilifuata taratibu za kisheria katika kuchagua njia ya zabuni ambazo zimewekwa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Ununuzi

Kiongozi wa jopo la mawakili wa Serikali, Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mlwambo awali aliweka pingamizi dhidi ya shauri hilo akiomba mahakama itupilie mbali huku wakitoa sababu nne, lakini Julai 25 mwaka huu upande wa Serikali uliamua kuondoa pingamizi.

Wakili Mlwambo akiwasilisha hoja za kuomba kuondoa pingamizi, alidai sababu kubwa ni kupisha usikilizwaji wa shauri mama na hakuna gharama kwa upande wowote.

Wakili Mpale Mpoki akiwawakilisha walalamikaji alikubaliana na hoja ya serikali kuondoa pingamizi, pia walijadiliana na wateja wao ambapo nao walikubaliana wakiwa na lengo la kuharakisha usikilizwaji na uamuzi wa shauri la msingi.

Walalamikaji katika shauri hilo wanapinga makubaliano yanayohusha uwekezaji katika bandari za Tanzania zilizoko katika mwambao wa bahari na katika maziwa, kuwa ni batili kwa kuwa yana ibara zinazokiuka sheria na Katiba ya nchi.

Wanadai makubaliano hayo yanahatarisha mamlaka ya nchi na usalama wa Taifa na kwamba yaliridhiwa na Bunge kinyume cha utaratibu bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao.

Makubaliano hayo yalitiwa saini Oktoba 25, 2022 na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, baada ya kupewa nguvu ya kisheria na Rais Samia Suluhu Hassan, huku Katibu Mkuu wa wizara hiyo, akishuhudia na yaliridhiwa na Bunge Juni 10, 2022.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Julai 25 mpaka Julai 28 mwaka huu, mawakili wa waombaji katika shauri hilo walimaliza kuwasilisha hoja zao huku wakidai mkataba unakiuka sheria na Katiba ya nchi.

## HABARI KITAIFA

### LHRC yatatua migogoro 1,500 ya mirathi miezi 6

**Na Halfani Chusi**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kimepokea jumla ya mashauri 1,531 ya migogoro ya mirathi, yakihusisha wanawake kwa asilimia 62 na wanaume asilimia 38 katika kipindi cha miezi sita.

Sababu kubwa imetajwa ni watu kutojenga utaratibu wa kaundika wosia na kukumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salam, Ofisa Sheria Dawati la Familia wa LHRC, Cajetan Matumaini, alibainisha hayo alipotoa maelezo ya shughuli mbalimbali kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro aliyetembelea ofisi za msaada wa kisheria kwa ajili ya kuangalia vikwazo vinavyowakabili wakati wa utoaji wa huduma hizo.

"Sababu nyingine ni ukosefu wa elimu kuhusu masula ya mirathi na wengine kujaribu kuvunja haki ya mwingine ili kupata mirathi kwa kulazimisha ilhali anatambua hana haki pamoja na ukosefu wa elimu ya mirathi kwa waathirika," alieleza.

Baada ya kupokea maelezo hayo, waziri huyo aliwataka watanzania kujenga utamaduni wa kuandika wosia, ili kuepusha migogoro ya mirathi pindi mtu anapofariki dunia na kwamba kufanya hivyo sio uchuro.

"Hivi vitu vinaendana na culture (utamaduni). Watanzania wengi hawana tabia ya kuandika wosia, lakini hawajui kila jambo tunalolifanya litakwenda zaidi ya muda wa kuishi.

# Kilio wenye maduka 19 yaliyoungua ajali ya lori

**Na Jenifer Gilla**

NI kilio kwa wenye vibanda 19 vya biashara na pikipiki zilizoteketea kwa moto juzi katika eneo la Kimara Kibo, jijini Dar es Salaam, baada ya lori lililokuwa limebeba mafuta kupinduka na kuwaka moto uliosambaa na kuteketeza maduka hayo.

Kama wamiliki walikuwa hawajakata bima za biashara zao, watabaki na kilio kwa kuwa ili walipwe fidia watatakiwa wawe na bima hiyo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kinondoni, Elisha Mugisha, aliiambia Nipashe kuwa walifanya tathmini na kugundua kuwa vibanda vilivyofikiwa na moto huo vilikuwa 19 na kusababisha uharibifu mdogo wa mali za wajasiriamali hao.

"Hakukuwa na madhara makubwa, wala haukuathiri mali zilizokuwa ndani ya maduka hayo zaidi ya vitu vidogo vidogo vilivyokuwa nje kama vile mabango ya matangazo ya biashara," alisema.

Alisema kuwa mpaka jana hawajapokea taarifa yoyote ya watu kupata majeraha yanayotokana na moto huo na hiyo imetokana na juhudi kubwa zilizofanyika kudhibiti mapema.

Meneja wa Kudhibiti Vihatarishi vya Bima wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Muyengi Zakaria, alisema tukio hilo linapaswa kuwakumbusha wafanyabiashara umuhimu wa kukata bima ili kujikinga wanapopata majanga kama hayo.

Alisema kwa sasa bima siyo jambo la starehe bali ni la muhimu kwa sababu linasaidia kupunguza mzigo wa hasara wakati mtu anapopatwa na majanga yasiyozuilika kama hilo la moto.

Aliwataka wafanyabiashara kutembelea ofisi za bima na kupata elimu na namna ya kukata bima ili kujiweka katika hali salama janga linapotokea.

"Tukiwa kama wasimamizi wa jambo hili, tunashirikiana na serikali na wadau wa bima kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha ukataji bima kupitia warsa, mikutano na shughuli mbalimbali, mwezi ujao tutakuwa na wiki ya bima lengo ni kuelimisha ukataji wa bima," alisema.

Meneja Mkuu wa kampuni ya bima ya FBN Insurance Broakers, Omari Azizi, alisema kama waliopatwa na janga hilo wamekata bima basi watalipwa gharama zao kulingana na kiwango walichokata.

Lori hilo lililokuwa limebeba mafuta likielekea Bukoba mkoani Kagera lilipinduka mita chache karibu na kituo cha mabasi cha Kibo na kusababisha moto mkubwa uliozua taharuki kwa wakazi wa eneo hilo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
07.08.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **11.08.2023 hadi 25.08.2023** kampuni ya CEVA Interfreight itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Dar Es Salaam kuelekea Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.0** |
| **Upana** | - | **Mita** | **7.50** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: Bandari ya **Dar Es Salaam hadi Mzenga** kupitia Barabara ya **Mandela**, Barabara ya **Morogoro mpaka Mlandizi,** magari yatasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga magari yatasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



## Tanzania Commercial Bank yawezesha Wadau wa Kilimo kwa riba na masharti nafuu

Sekta ya kilimo nchini inachangia asilimia 28.7 kwenye Pato la Taifa (GDP) na vilevile huchangia nguvu kazi ya Taifa kwa ajira za moja kwa moja kwa asilimia 65.5, huku ikichangia asilimia 10 ya kazi zisizo moja kwa moja.

Hata hivyo, kati ya taasisi za kifedha 24 nchini zilizofanyiwa utafiti, benki 13 ziligunduliwa kuwa na bidhaa au huduma za utoaji mikopo kwa wakulima (kwa mujibu wa utafiti wa FSD Tanzania).

Kwa umuhimu wa sekta hiyo, Benki ya Bishara Tanzania (TCB) iliona umuhimu wa kuwadumia wakulima nchini katika huduma na bidhaa zake na hivyo kuanzisha kitengo kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima ili kuweza kuwapatia fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kilimo kama mitaji, matumizi ya kuendeshea shughuli za kilimo na shughuli baada ya mavuno.

Hii imekuwa njia moja wapo ya kusaidia wakulima na pia juhudi za serikali katika kuhamasisha kilimo biashara nchini.

Mikopo ya kilimo biashara ya TCB kwa sasa inalenga sekta ya kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali muhimu kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na taasisi ya Private Agriculture Sector Support (PASS) na pia Alliance for Green Revolution in Africa.

Mikopo inayotolewa na benki ya TCB kwa ni kwa ajili ya wakulima wadogo (small holder farmers), wajasiriamali wadogo na wakati (SME's) na hata wale wa juu wanaojihusisha na maswala mbamlimbali katika sekta ya kilimo kama wazalishaji wadogo, wakusanyaji nafaka, wasindikaji na wasambazaji wa pembejeo, pia na sekta ya uvuvi, ufugaji wanyama na misitu.

Banki ya TCB imesema kuwa imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia wakulima wa aina zote nchini katika swala la kutoa mikopo na hivyo kuwashauri wateja wake kutembelea kwenye matawi yao yaliosambaa nchi nzima ili kufaidika na huduma zinazotolewa na TCB.

Hayo alisemwa na Meneja wa Mikopo kutoka TCB, Lucius Mtewele wakati akiongea na Nipashe kuelekea kilele cha sikukuu ya wakulima ya Nanenane ambayo huazimishwa nchini kila tarehe 8 mwezi Augusti kila mwaka.

Mtewele alisema kuwa benki hiyo imejikita katika kutoa elimu na fedha kama mikopo nafuu na rafiki kwa wakulima na wadau wote katika mnyororo wa thamani kuhakikisha kuwa wanawezeshwa kufanya kilimo biashara chenye tija kwa uchumi wao na wananchi kwa kiujumla.

Mtewele alisema kuwa mwamko umekuwa chanya kwa katika swala la mikopo kwa wateja wa kilimo hasa wakulima wadogo ambao awali hawakuweza kufikiwa na na huduma za kifedha.




"Wakulima wadogo wamekuwa wakijitokeza zaidi kwa sababu ndio kundi ambalo linauhitaji mkubwa na hawakuwa wamefikiwa na huduma hii" alisema Mtewele.

Mtewele alisema kuwa sekta ya kilimo biashara inakuwa kwa kasi sana, kwani wakulima wameendelea kupata huduma za kifedha kitu ambacho kimekuwa kichocheo kikubwa katika ukuaji wa kilimo vilevile ni sekta pekee inayokuza uchumi kwa upana na jumuishi ukilinganisha na sekta nyingine.

Aliongeza kuwa mikopo ya kilimo inatolewa matawi yote nchini, bara na visiwani na inachukua mda mfupi iwezekanavyo ili kumwezesha mkulima kufanya shughuli zake kwa wakati sahihi.

"TCB inaendelea kupanua wigo wa upatikanaji huduma za kifedha kwa wakulima, ikiwa ni pamoja na kuwafikia wakulima walioko vijijini, kutoa fursa kwa makundi muhimu kama vile vijana na wanawake" aliongeza Mtewele.

Mtewele alisema kuwa mikopo ya kilimo ya TCB ni tofauti na mikopo kutoka taasisi zingine za kifedha sababu ni jumuishi kuanzia wakulima wadogo wa kati na wakubwa.

"Si hayo tu lakini pia mikopo yetu ina gharama nafuu, na inapatikana kwa uharaka na zaidi mikopo hiyo inatolewa kwa wadau wote kuanzia wadau wa kilimo shambani, wanunuzi mazao, waongeza thamani, wauzaji wa pembejeo na wadau wengine kwenye mnyororo wa thamani, tupo kwa ajili yao na tupo kwa ajili ya kuwahudumia" alisema Mtewele.

# Usafishaji kucha mitaani unavyobeba hatari kiafya

**Na Jenifer Gilla**



KUSAFISHA na kupaka rangi kucha sasa ndiyo habari ya mjini kwa wanawake na wasichana! Lakini nyuma ya huduma hiyo kuna hatari za kiafya, pamoja maradhi ya kuambukiza kama vile Virusi vya Ukimwi (VVU), fangasi na bakteria ikiwa usalama wa vifaa hautazingatiwi.

Usafishaji kucha unahusisha matumizi ya vifaa vya kukata kucha (nail cutter), kuchokonoa na kuondoa uchafu katika kucha (nail filer), vilevile vipo vya kupaka rangi.

Udadisi wa Nipashe katika baadhi ya saluni zilizozagaa mkoani Dar es Salaam, sambamba na kwa watoa huduma hiyo wasio na vituo maalum wanaopita nyumba kwa nyumba, umebaini baadhi yao hawazingatii kanuni na tahadhari za kiafya.

Nipashe imebaini wanapotoa huduma hiyo, hutumia kifaa kimoja cha kusafisha kucha, kuwahudumia wateja kadhaa, mhusika mmojawapo, ambaye mwongozo wake kuisha makali ya kifaa chake, akikadiria idadi ya wateja wake kwa kauli "hunichukua siku mbili hadi tatu kubadilisha kifaa".

Uchunguzi wa mwandishi wa habari hizi, umebaini kwamba, wakati kifaa kinauzwa kwa bei ya wastani Sh. 1,000, huduma zinazotolewa kwa mteja ni wastani wa Sh. 2,000 hadi 5,000 kutegemeana na aina ya huduma inayotolewa.

Katika saluni ya kike iliyoko Vingunguti, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, mwandishi alimkuta msafishaji kucha Said Mahmoud wiki iliyopita, akitoa huduma kwa mteja wake kwa kifaa ambacho alishakitumia kwa mteja mwingine.

Namna anavyotumia vifaa hivyo, Mahmoud alisema kwa kawaida anabadilisha kifaa cha kutolea uchafu katika kucha baada ya siku mbili, wakati cha kukatia kucha hubadilisha anapohisi kimeisha ukali.

Mahmoud ambaye alijitambulisha hutembelea saluni mbalimbali za kike jijini kutoa huduma hiyo kwa wateja, anasema kwa siku hutoa huduma kwa wastani wa wateja 15 katika maeneo ya Vingunguti, Tabata, Buguruni na Ilala.

Mwandishi alipohitaji kujua hadhari za kiafya dhidi ya usalama wa vifaa, Mahmoud alibainisha kuwa kati ya wateja hao, ni wastani wa wateja watatu anaowakuta na vifaa vyao, wengine anawahudumia kwa kutumia kifaa chake.

Mahmoud pia alikiri kufahamu madhara ya kiafya kutokana na kuchangia vifaa hivyo, akitamka: "kunaweza kueneza fangasi, ila siyo jukumu langu kumnunulia kila mteja kifaa hicho.

"Unajua kila kitu kinaanza na mteja mwenyewe. Kama wanaridhika kutumia kifaa hiki, mimi nifanye nini? Sina uwezo wa kutoa Sh. 1,000 kumnunulia kila mteja kifaa chake ilhali wanalipa Sh. 2,500 tu kwa huduma ninayowapa. Wanapaswa wao wenyewe wanunue vifaa hivyo."

> **Kwahiyo, hata ukisema umwagize inakuwa kazi bure, maana kama ukija tena saluni utamkuta mwingine. Hivyo, tunatumia tu hivyo vyao.**

Naye Steven Michael anayetoa huduma hiyo huko Mwenge, wilayani Kinondoni, anasema tatizo liko kwa wateja wao, anaowataja kuwa wengi wao ni wanawake. Hawaoni umuhimu wa kujinunulia vifaa hivyo.

Anabainisha kuwa katika eneo lake la kazi, vifaa hivyo vipo kwa wingi na bei yake ni nafuu, lakini wapo wateja ambao hawanunui mpaka walazimishwe licha kufahamu madhara yake kiafya.

"Kwa mfano, mimi sina hivi vifaa. Kwahiyo, mteja anayekuja kwangu ni lazima ajinunulie kifaa chake ambacho kinauzwa kwa buku (Sh. 1,000) tu. Lakini kati ya wateja 10 wanaokuja kwangu, unakuta watatu wanaondoka kwa kuwa sina vifaa hivyo. Wanakwenda sehemu kuliko na vya kuchangia. Sasa unaona tatizo lilipo," Steven anafafanua.

Ni hoja inayoungwa mkono na Lameck Bazir, anayetoa huduma hiyo Tandika, wilayani Temeke, anayesema kununua vifaa vya kusafisha kucha kunapaswa kufanywa na mteja kwa kuwa malipo ya huduma ni nafuu.

"Unajua sisi wa huku uswahilini, huduma hii tunaitoa kwa bei nafuu sana. Hivyo, mteja anapaswa kujinunulia vifaa hivyo ambavyo atavitumia zaidi ya mara moja.

"Ni suala la kujitambua tu kwa sababu katika saluni za Masaki huduma hii inatolewa kwa zaidi ya Sh. 15,000 na bado mteja ananunulia mwenyewe vifaa," anadai.

Ili kukabiliana na hatari ya kiafya iliyopo kutokana na kuchangia vifaa, Bazir anashauri wanatoa huduma hiyo wawe na kauli moja. Wakubaliane kupandisha bei ili wawanunulie wateja vifaa hivyo. Itapunguza hatari ya kuambukizana maradhi.

Mkazi wa Tabata, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, Jamila Steven, anakiri hupata huduma hiyo mara moja kwa wiki na hajawahi kujinunulia vifaa hivyo kwa kuwa anaamini havina madhara yoyote kiafya.

Jamila ana hoja nyingine ya kujitetea - anakosa muda wa kununua vifaa hivyo. Maduka ya urembo yako mbali na eneo analoishi na wanaotoa huduma hiyo anakoipata hawaviuzi.

"Unajua hawa watengeneza kucha tunakutana nao katika saluni tu, na siyo kila ukija hapa utamkuta huyuhuyu. Wakati mwingine unakuta mtu mwingine.

"Kwahiyo, hata ukisema umwagize inakuwa kazi bure, maana kama ukija tena saluni utamkuta mwingine. Hivyo, tunatumia tu hivyo vyao. Ninaamini Mungu atatunusuru na maradhi," anasema Jamila.

Latifa Iddy, mkazi wa Mbagala, wilayani Temeke, anaamini kwamba wateja wa huduma hiyo kutokuwa na elimu ya afya, kunasababisha wengi wao kukubali kuchangia vifaa hivyo.

"Wengi tunaamini magonjwa ya kuambukizwa yanaenezwa kupitia matendo maovu na ya muda mrefu kama vile ngono zembe, jambo ambalo siyo kweli.

"Wanawake wengi wanasumbuliwa na kukosa maarifa, mtu anakidharau kifaa cha kusafishia kucha kwa kuwa ni kidogo. Haamini kama kinaweza kumwambukiza VVU.

"Mimi binafsi nina kifaa changu, ninatembea nacho kwenye pochi. Kuna haja kutoa elimu katika saluni juu ya suala hili," anashauri Latifa.

## MATABIBU WANENA

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Agakhan, Willbroad Kyejo, anafafanua kitaalamu kwamba, kuchangia vifaa katika huduma hiyo ni hatari. Kuna uwezekano wa kupata maambukizi ya kuvu na bakteria.

"Pale ambapo zana za kukata kucha hazisafishwi vya kutosha kati ya wateja, vimelea hatarishi vinaweza kusambazwa kirahisi, kusababisha maumivu na maambukizi yasiyoridhisha.

"Maambukizi ya kuvu kwenye kucha na paronychia ya bakteria (kuvimba kutokana na kiwewe, kuwasha au maambukizi) ni matokeo ya kawaida ya mazoea mabaya ya usafi katika saluni za kucha," Dk. Kyejo anafafanua.

Anaonya kuwa kuchangia vifaa hivyo, hasa vyenye ncha kali, kunaweza kusababisha maambukizi ya maradhi ya ngozi kama vile fangasi na VVU ikiwa kilitumika na kumkata mgonjwa mwenye maambukizi hayo.

Mkuu wa Idara ya Ukunga na Afya ya Uzazi katika Hospitali ya Taifa Muhimbli (MNH), Dk. Priscilah Kinyamagoha, anatoa angalizo kwamba, kuchangia vifaa hivyo kuna madhara mengi kiafya.

Kama ilivyo kwa mtangulizi wake Dk. Kyejo, Dk. Priscilah, anaonya tabia hiyo si salama kiafya, akisema: "...unaweza kupata magonjwa ya ngozi, fangasi, bakteria. Ukiacha kuchangia vifaa hivyo, utakuwa umejiepusha na magonjwa mengi sana."

Dk. Kyejo anaporejewa kuzungumzia hatua za kukabiliana na hatari hiyo, anashauri wanaopenda huduma hiyo kuchagua saluni zenye sifa nzuri zinazojali afya kwa kufuata protokali sahihi za kusafisha vifaa na kujinunulia vifaa vyao ili kuepuka maambukizi ya magonjwa.

Vilevile, anashauri wanaotoa huduma hizo kupata elimu ya namna ya kuwahudumia wateja na utumiaji vifaa hiyo kwa kuwa wengi wanajifunza kupitia kwa wenzao na siyo kwa wataalamu wa kucha.

"Na hili ndilo tatizo kubwa. Kama amejifunza kupitia kwa mwenziwe ambaye naye hajui umuhimu wa kutochangia vifaa hivyo, na yeye atafuata njia hiyo.

"Kwahiyo, ni muhimu waende kupata elimu katika shule za urembo ili wapate na elimu sahihi ya afya," anashauri bingwa huyo.

Dk. Priscilah anaungana na daktari mwenzake kusisitiza wanawake wanaopenda kupata huduma hiyo, wasividharau vifaa hivyo kwa kuwa madhara yapo na kuwasihi kujijengea utamaduni wa kununua vifaa vyao na kutembea navyo katika mapochi zao.

"Kama mtu anaweza kupaka rangi kwa Sh. 3,000 hadi 10,000, anashindwaje kununua kifaa chake mwenyewe kwa Sh. 1,000 ili apate huduma akiwa katika mazingira salama kiafya?" Dk. Priscilah anahoji.

Ofisa Tabibu katika Kituo cha Afya cha One Health Polyclinic, Dk. Abel Nandonde, anashauri inaposhindikana kubadilisha vifaa hivyo, vilivyopo visafishwe kitaalamu baada ya kumhudumia mteja ikiwamo kuvichemsha na kutumia dawa za kuua vijidudu, ili kuzuia maambukizi kama wanavyofanya wenye saluni za kiume.

# Mpango azidi kulia na mmomonyoko wa maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema kama hatua za haraka hazitochukuliwa kudhibiti vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwa vijana nchini, taifa litakuwa katika wakati mgumu kupata viongozi waadilifu wa kuliongoza.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua kongomano la siku mbili la vijana lililoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kujadili fursa na vikwazo kwa vijana katika kujikwamua kiuchumi.

"Maadili kwa vijana hivi sasa ninasikitika kusema yameporomoka sana vijana wamekuwa siyo waadilifu. Wanafanya vitendo visivyofaa. Vijana hawana utii wa serikali yao, siyo waaminifu, hawana utii wa sheria za nchi, wapenda rushwa, hawana bidii ya kazi, wanataka utajiri wa haraka.

"Vijana wakikosa uadilifu, hatuwezi kupata viongozi waaminifu ambao wataliongoza taifa letu kwa uaminifu. Jambo lingine baya zaidi ni matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana pamoja na ndoa za jinsia moja. Inatupasa kuchukua hatua za haraka kukabilina na hali hii ili kuokoa taifa letu," aliagiza.

Dk. Mpango ambaye hivi karibuni alikemea vikali vitendo vya ndoa za jinsia moja, alisema kukosekana uaminifu kwa vijana kunawafanya washindwe kuijenga Tanzania ya sasa na kesho licha ya kuwa wao ndiyo wanategemewa wakati wazee watakapokuwa wamechoka.

Alisema baadhi ya vijana wamejikita katika rushwa na utapeli, wengine wamejiingiza kwenye mapenzi ya jinsia moja ambayo ni kinyume cha maadili, mila na tamaduni za kitanzania.

Alitoa maagizo matano kwa halmashauri nchini ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha vijana katika uzalishaji mali na kuwa na kanzidata za kuwatambua vijana na sifa zao kitaaluma.

Maagizo mengine ni halmashauri kutenga maeneo ya kufanyia biashara na kuyatangaza hadharani, kuwaunganisha vijana na fursa zinazowazunguka kwa uwazi na elimu lakini vijana waunde klabu za mazingira kila maeneo ili wasaidie kupambana na uharibifu wa mazingira.

Pia alimwagiza Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, kuandika barua kwa wakuu wa mikoa kote nchini kuiga mfano wa Dodoma na kuandaa makongamano ya vijana na kuwapa fursa za kujadili mambo yao.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alitaja makundi ya vijana walioshiriki kongamano hilo ni pamoja na wajasiriamali, VETA, wanufaika wa mikopo ya asilimia 10, JKT, Mgambo, bodaboda, machinga na vijana walioko katika mafunzo ya miradi ya kilimo ya BBT.

# MSD kuokoa bil. 33/- kukamilika kiwanda cha mipira ya mikono

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BOHARI ya Dawa (MSD), inatarajia Septemba, mwaka huu kuanza uzalishaji wa mipira ya mikono kwenye kiwanda chake Idofi mkoani Njombe, kitakachookoa Sh. bilioni 33 zilizokuwa zikitumika kuagiza mipira hiyo nje ya nchi.

Meneja Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini wa MSD, Hassan Ibrahim, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bohari na mwelekeo wa mwaka 2023/24.

Alisema katika kufanikisha ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za afya nchini na kuendana na azma ya serikali ya uanzishaji wa viwanda, MSD ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha miundombinu ya kiwanda hicho kitakachotoa ajira za moja kwa moja kwa watu takribani 200.

"Kiwanda cha uzalishaji mipira ya mikono kitachagiza uzalishaji wa malighafi ya mpira hapa nchini na kupunguza utegemezi kutoka nje ambapo fedha za kigeni sawa na Sh. bilioni 33 ambazo hutumika kila mwaka kuagiza mipira ya mikono nje ya nchi," alisema.

Aidha, alisema katika kuendana na kasi ya ongezeko la vituo vya afya inayofanywa na serikali, bohari imekuwa ikifanya mawasiliano na balozi zilizopo China, Algeria, Korea ya Kusini, Urusi na maeneo mengine duniani ili kuwatambua wazalishaji, wawekezaji ili ununuzi wa bidhaa za afya kwa uhakika, ubora na gharama nafuu.

Kadhalika, alisema kwa mwaka 2023/24 MSD imejipanga kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya na miundombinu ya utunzaji wake na kwamba ujenzi wa maghala unatarajiwa kuanza Agosti 2023 katika mikoa ya Dodoma, Mtwara na Kagera ili kuongeza nafasi za kuhifadhi bidhaa na kuimarisha ubora wa bidhaa za afya.

Pia, alisema MSD ipo kwenye maandalizi ya awali ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha dawa na bidhaa za pamba tiba.




Meneja Mauzo wa Tigo Mbeya, Fadhila Said (kushoto), akitoa maelezo kuhusu huduma za intaneti kwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alipotembelea banda la Tigo katika maonyesho ya wakulima Nane Nane viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jopo madaktari bingwa mifupa Marekani kuweka kambi nchini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JOPO la madaktari bingwa 60 wa mifupa kutoka nchini Marekani, wanatarajia kuweka kambi ya siku saba mkoani Arusha kutoa huduma ya matibabu ya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa wasiojiweza na wanaotoka familia maskini.

Timu ya madaktari hao ambao ni wageni maalum wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wataanza rasmi kutoa huduma hizo za matibabu katika Hospitali ya Seliani jijini hapa kuanzia Agosti 11 hadi 17, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, mdau wa maendeleo ambaye aliyewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu, alisema wageni hao wameitikia wito wa Rais kutokana na uhusiano uliojengwa kati ya nchi ya Tanzania na Marekani pamoja na kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

"Wamekubali kuja kujitolea kwa gharama zao kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji mahususi kwa magoti na nyonga na ugeni huu ni wa kihistoria kwa kuwa hivi karibuni alikuja Makamu wa Rais Marekani, pia Rais wetu alikwenda huko na nchi nyingine katika hatua ya kujenga uhusiano wa kimataifa.

"Kutokana na uhusiano wa kimataifa aliojenga Rais Samia, kilichotokea madaktari bingwa kweli kweli 60 watakaa na sisi kwa takribani siku saba hapa Arusha na watatibu wenye matatizo ya nyonga na magoti.

Nyalandu, alisema Rais Samia ameelekeza wagonjwa watakaopewa kipaumbele ni wale wanaotoka familia maskini na wasiojiweza kwa kuwa hawana uwezo wa kukidhi gharama za matibabu na huduma watapatiwa bure.

Hata hivyo, alisema kutokana na mazungumzo aliyofanya na jopo na madaktari hao, walimweleza kuwa gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja ni kuanzia Dola za Kimarekani 30,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 70.

"Tunasema huu ni upendo wa mama na kinachoendelea Arusha na kwa Kanda ya Kaskazini wamepewa upendeleo wa upekee ingawa wagonjwa wanatoka mikoa yote nchini bila kujali dini, kabila au chama cha siasa," alisema Nyalandu.

Alisema Agosti 10 mwaka huu, mapokezi maalumu yatafanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), siku watakapowasili na kutakuwapo kwa ujumbe wa serikali.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Seliani, Dk. Goodwill Kivuyo, alisema kama hospitali wamefurahia kupata fursa ya kuwapokea wageni hao ambao ni wa kiongozi mkuu wa nchi.

Alisema mpaka jana walikuwa wameshasajili wagonjwa zaidi ya 200 kwenda kuwaona madaktari ili wafaidike na huduma hiyo.

"Huduma itahusisha sana wagonjwa ambao wenye magonjwa ya goti waliokuwa na maumivu ya kudumu sana na magonjwa mengine yaliyoshindikana ikiwamo ya nyonga watanufaika na huduma hiyo," alisema Dk. Kivuyo.

Pia, alisema wanatarajia baada ya kambi hiyo kufikia tamati umma wa Watanzania watakuwa wamepata huduma hizo kwa kiasi kikubwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi msikimbilie majanga jifunzeni kuepuka

**JUZI** katika eneo la Kimara Kibo wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, kulizuka taharuki kubwa baada ya lori la mafuta kupinduka na kuwaka moto.

Tukio hilo lilisababisha barabara ya Morogoro ambayo hutumika sana kwa magari yaendayo mikoani kusimama kwa saa kadhaa baada ya lori hilo kufunga njia.

Yanapotokea matukio kama hayo kumekuwa na kawaida ya wananchi kukimbilia kwa nia ya kushuhudia kinachotokea jambo ambalo ni hatari linaloweza kusababisha vifo vingi.

Kwa tukio la juzi Mungu ashukuriwe halikusababisha vifo isipokuwa uharibifu wa vibanda vya wafanyabiashara vilivyojengwa karibu na barabara.

Matukio kama haya ya kupinduka magari ya mafuta huleta majanga makubwa kwa sababu wananchi hukimbilia kwenda kuchota mafuta bila kujali madhara yake.

Wengi watakuwa hawajasahau tukio lililotokea mkoani Morogoro baada ya lori la mafuta kupinduka na watu kukimbilia kwenda kuchota mafuta na kuishia kuteketea kwa moto.

Watu wengi walipoteza maisha katika tukio lile, lakini bado inashangaza kuna baadhi hawakumbuki madhara hayo na wana uthubutu wa kwenda kujitosa kwenye hatari hiyo.

Pamoja na vyombo husika kutoa elimu kuhusu madhara ya kukimbilia majanga, bado watu wanaziba masikio na kujitosa.

Baadhi yao hugeuka waandishi wa habari na kupiga picha matukio huku wakiwa wamekaribia eneo la hatari.

Kila kazi ina mafunzo yake, waandishi wa habari hawawezi kukaribia tukio la hatari bila kupata maelekezo kutoka kwa Jeshi la Zimamoto au Kikosi cha Usalama Barabarani.

Vilevile wanapokwenda kwenye matukio hayo wanakuwa na vifaa vya kuwakinga ili wasidhurike.

Katika nchi zingine wananchi wanapoona matukio ya hatari kama hayo hukimbia na kukaa mbali kuepusha majanga.

Kuna tukio lililotokea nchini wakati Ubalozi wa Marekani ulipolipuliwa kwa mabomu jijini Dar es Salaam, wananchi walitoka sehemu mbalimbali na kukimbilia kwenye ubalozi kushuhudia mabomu yanavyolipuka.

Watu wengi waliumia na kupoteza maisha kwa sababu ya kukimbilia eneo lenye hatari badala ya kuikimbia.

Tukio pia la kulipuka mabomu lililotokea maeneo ya Ukonga, jijini Dar es Salaam, lilitetemesha jiji na baadhi ya watu walithubutu kukimbilia huko ili washuhudie.

Watanzania wanahitaji elimu ya mara kwa mara kukumbushwa kuwa yanapotokea majanga kama ya ajali za magari ya mafuta hawatakiwi kukimbilia na badala yake wakimbie na kuwa mbali nayo.

Wengine hufariki siyo kwa kuungua na moto tu bali mvuke wa gesi unaotoka kwenye mafuta hayo huwafanya washindwe kupumua na matokeo yake hupoteza maisha.

Inawezekana wananchi hukimbilia kuangalia matukio hayo kwa kutaka kutoa msaada au wengine huenda kwa nia ya kuiba vitu, lakini mwisho wake wote hupoteza maisha.

Kazi ya uokoaji iachwe kwa vikosi maalumu vyenye utalaamu wa kuokoa yanapotokea majanga ya moto.

Na kuna wanaokwenda kuwahi mafuta yanayomwagika kwa nia ya kwenda kuyauza. Hiyo ni hatari kwao kwa sababu madhara watayayopata baada ya kuungua na moto ni kifo au kuuguza majeraha ambayo yanagharimu pesa nyingi. Na hata kama atapona ataishia kubaki na ulemavu wa maisha.

Ni vizuri Watanzania kujifunza kutokana na yaliyokwishatokea na kuona madhara yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Antoni Manjoro, TUDARCO

## Muungwana Lazima Nilonge

# Vijana wahamasike waanze kulima mijini

**MVUA** zinanyesha laiti zingetumiwa kwa tija. Ndivyo unavyoweza kusema ukiangalia mapori na mashamba yaliyoko mijini hasa majiji na miji mikubwa kama Dodoma, Dar, Mwanza na Tanga.

Unajiuliza kwanini watu wasilime? Mbona kuna mvua nyingi na mapori na mashamba ambayo ni viwanja vya watu ambayo hayajajengwa yako mengi kila mahali kwenye miji yetu.

Ndiyo maana naona kuna kila sababu ya serikali kushauri na kuwahimiza Watanzania hasa wanaoishi mijini kulima mazao kama mihogo, kunde, mbaazi, choroko, viazi na mboga kuanzia matembele hadi mhogo pia kwa ajili ya mboga.

Mvua zinazoendelea kunyesha kipindi cha sasa zinasaidia kutunza mazao hivyo, hawatahitaji kumwagilia mazao ya muda mfupi kama kunde, choroko na hata jamii za mboga kama matembele. Yote hayo yatapunguza ugumu wa maisha na matatizo ya njaa hasa kushindwa kupata mboga kunakotokana na kutokujishughulisha kwa wakazi wa mijini.

Viongozi wa kisiasa kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo na hata wale wa serikali za mitaa waanze kutoa elimu juu ya namna bora ya wananchi kujishughulisha na kilimo ili kupunguza ugumu wa maisha na kukosa chakula.

Ni ajabu mvua kunyesha hadi kumalizika lakini mashamba au viwanja ambayo havijajengwa vikiwa vimejaa nyasi lakini si mihogo wala mbaazi au kunde.

Yaliyopita si ndwele mambo yaanze sasa, viongozi watoe mapendekezo kwa wamiliki kuwa sehemu ambazo hazijajengwa na mapori ambayo huf-uga nyoka , vibaka na majambazi wananchi waandaliwe utaratibu wayatumie kuzalisha chakula mijini.

Ni vema wangetumia fursa hiyo kwani itasaidia katika kujipatia kipato na chakula kwa wananchi hasa kipindi hiki cha mvua hasa kwa wakazi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa jiji na majiji.

**Ni wazi kuwa wakazi wengi wa mijini hasa Dar es Salaam wamekuwa wakijikita katika shughuli za biashara kuliko kilimo kutokana na mazoea lakini pia kilimo kinaweza kupewa nafasi na kubadili maisha ya wananchi.**

Kipindi hiki mvua zimekuwa zikinyesha katika maeneo mengi mathalani Dar es Salaami, hivyo maeneo ambayo hayajajengwa yangetumika katika kuendesha kilimo cha mazao ya muda mfupi ya chakula na biashara.

Ninayasema haya kwani nimeshuhudia katika masoko kadhaa kama Tandika mkoani Dar es Salaam, mboga za majani huagizwa kutoka mikoani kwa mfano Iringa, Morogoro na Pwani na wauzaji wakieleza kuwa kiwango kidogo kinachozalishwa mijini mfano Dar es Salaam hakitoshelezi mahitaji ya wateja.

Lakini pia katika soko la Mabibo ni miongoni mwa masoko yanayoleta mazao ya muda mfupi kama vile nyanya vitunguu na ndizi kutoka mikoani, inawezekana ni sawa kibiashara, lakini wakazi wa mijini wana jukumu la kuzalisha pia.

Ningeomba serikali iweze kutumia nafasi hii ya sikukuu ya Nane Nane ya kuwapongeza wakulima kutoa elimu ya kilimo kwa wakazi wa mijini itakayoendana na kufahamu umuhimu wa kutumia mvua zinazoendelea kunyesha.

Lakini pia serikali itoe maagizo kuwa maeneo hasa viwanja, mashamba na mapori ambayo hayajaendelezwa yatumike kwa tija na wakazi watakaojihusisha na kilimo hicho.

Ni wazi kuwa wakazi wengi wa mijini hasa Dar es Salaam wamekuwa wakijikita katika shughuli za biashara kuliko kilimo kutokana na mazoea lakini pia kilimo kinaweza kupewa nafasi na kubadili maisha ya wananchi.

Mwaka huu umekuwa na mvua nyingi za masika lakini kutokana na kukosa hamasa ya kulima mapori na viwanja ambavyo havijaendelezwa yamebakia kuwa vichaka badala ya kujaa mihogo, viazi, mbaazi na mhogo mpira kwa ajili ya kisamvu.

Kadhalika maeneo hayo yanafaa kupandwa matunda kama mapapai ambayo hayahitaji kumwagiliwa na hata matango na matikiti iwapo mkulima ana chanzo cha maji karibu.

HABARI KITAIFA

# Michango shuleni yashtua uongozi

Na Pilly Kigome

MKUU wa Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Edward Mpogolo, amewaagiza maofisa elimu msingi na sekondari kutembelea na kukagua shule ili kubaini zinazochangisha wanafunzi michango ambayo siyo rasmi.

Ni hatua aliyochukua baada ya wananchi wa Segerea kupeleka malalamiko yao kwa mbunge wao, Bonna Kamoli, kumwomba alifanyie kazi suala hilo ambalo naye akaliwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya.

Alisema wazazi wa jimbo hilo wanalalamikia kuteswa na michango ambayo inawanyima usingizi na watoto wao kurudishwa nyumbani pindi wanapokosa fedha za michango.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika jana Kata ya Buguruni ukihusisha kata tano za Buguruni, Mnyamani, Vingunguti, Kiwalani na Minazi Mirefu, Mkuu wa Wilaya Mpogolo alisema serikali imeshatoa tamko kuwa elimu ni bure kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema kusiwe na watu wanajichukulia au kujitungia sheria zao ambazo zinakwenda kinyume.

Mbali na michango midogo ya Sh. 200 hadi Sh. 500, kiongozi huyo pia alitoa katazo la mtindo wa walimu kuwatoza wanafunzi fedha za kufanyia mitihani inayofanywa baadhi mara tatu kwa wiki ikiwa ni kinyume cha utaratibu.

"Ninatoa tamko leo - wanafunzi hafaulu kwa kumfanyisha mitihani kila siku. Michango hii hairuhusiwi kisheria. Kwanza; mwanafunzi anafanya mtihani Jumatatu, Jumatano anafanya mtihani mwingine, hao walimu wanasahihisha muda gani? Mwanafunzi leo kafanya mtihani, kesho anafanya, hii haiko sawa.

"Ni lazima tuweke mipaka ya michango, na michango inayoruhusiwa ya kuchangia mitihani ni ile ya mwisho wa muhula na si kama wafanyavyo. Hii ni kero kubwa kwa wazazi na tutambue sasa hivi maisha ni magumu," alisema.

Kiongozi huyo aliwakumbusha wazazi kuwa wajibu wao ni kuhakikisha mtoto anakula, anakunywa na analala, hivyo wafike shuleni kuonana na kamati za shule na si walimu ili kuhakikisha wanaliongelea hilo kwa upana.

Meya wa Jiji Ilala, Omari Kumbilamoto, aliwataka wananchi kuendelea kuwa na imani na serikali kwani ina mipango mizuri ya kuendeleza nchi ikiwamo na kutekeleza ilani zilizowekwa kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alimpongeza Mbunge Kamoli kwa juhudi zake kubwa anazofanya kuleta maendeleo katika jimbo hilo ikiwamo na kusimamia ujenzi wa shule za msingi na sekondari, vituo vya afya barabara 46 jimboni.

Mbunge Bonna alipongeza serikali kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi wake hususani katika jimbo hilo. Anahisi faraja na hamasa kutumikia wananchi kutokana na juhudi zinazoonyeshwa.

## eGA yazitaka taasisi za umma kujiunga na mfumo wa GovESB

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imezisisitiza taasisi za umma kujiunga na mfumo wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GovESB) utakaorahisisha kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali ili kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati.

Meneja Mawasiliano wa e-GA, Subira Kaswaga, alitoa rai hiyo jana katika maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.

Alisema mfumo wa GovESB ni shirikishi na unawezesha taasisi za umma kuunganisha mifumo yao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kupitia mfumo huo ili kuzungumza na kubadilishana taarifa kidijitali.

Alibainisha faida za mfumo huo ni pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma, kuokoa muda, gharama za uendeshaji wa taasisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa wakati.

"Mfumo wa GovESB ni jitihada za mamlaka za kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inazungumza na kubadilishana taarifa ili kupunguza urudufu wa mifumo serikalini.

"Kwa sasa, taasisi mbalimnbali za umma zimeunganisha mifumo yake na GovESB lakini zipo taasisi ambazo bado hazijaunganisha, hivyo nitoe wito kwa taasisi hizo kujiunga na mfumo huu wa GovESB," alisema Kaswaga.

Ofisa TEHAMA wa e-GA, Caesar Mwambani, alisema kuwa mamlaka hiyo kwa kushirikiana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetengeneza mfumo wa e-Mrejesho unaowawezesha wananchi kuwasiliana na serikali kidijitali.

**Mfumo wa GovESB ni jitihada za mamlaka za kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inazungumza na kubadilishana taarifa ili kupunguza urudufu wa mifumo serikalini.**



Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba (wa pili kulia), akimkabidhi kitabu chenye miongozo mbalimbali ya mfuko huo, Mkurugenzi wa Usimamizi Raslimali Watu na Utawala wa Benki Kuu, Kened Nyoni, alipotembelea banda la benki hiyo kutoa elimu na kuwahudumia. Wengine ni Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana, Isack Kijwili (kulia) na Meneja Msaidizi Idara ya Mawasiliano, Noves Moses. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC apongeza JCH kusaidia watoto mazingira magumu

Na Halfani Chusi

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo ameishukuru Nyumba ya Watoto ya Jerusalemu (JCH) kwa kuwekeza nguvu na kuwajali watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Halima alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki hii waliposhiriki mbio za marathoni zilizoandaliwa na JCH kwa ajili ya kuchangia watoto wenye uhitaji.

Alisema JCH, chini ya uongozi wa Mkurugenzi wake, Upendo Ngoda, imekuwa mwangaza wa kweli kwa watoto wanaohitaji ulinzi katika jamii.

Halima alisema kila rangi za nguo walizovaa zinaashiria kitu ambacho wamelenga kuchangia kwa ajili ya watoto hao; njano inasimama kwa ajili ya bima ya afya, kuhakikisha watoto wanapata huduma za afya wanazohitaji ili kukua na kuwa na afya njema.

"Kijani inawakilisha elimu, kuwawezesha watoto hawa kutimiza ndoto zao na kufikia mafanikio, nyekundu inaashiria azma yetu ya kujenga mustakabali bora kwa JCH, mahali ambapo ndoto si tu zinalelewa bali kutimizwa pia.

"Njia ambayo JCH, imechukua si rahisi, lakini safari hii ni ya thamani ningependa kuwahakikishia kuwa msaada kutoka kwa jamii, upendo kutoka kwa wafadhili waliojitolea, na moyo usiochoka kutoka kwa wafanyakazi wa JCH utatupeleka kule tunapopataka," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema tunaweza kufikia mafanikio makubwa na kutoa fursa wanazostahili watoto, akiwaambia watoto walioku wa wamekusanyika eneo hilo "nyinyi ndio tumaini la kesho, na ndoto zenu ni za thamani kubwa.

Pia aliwashukuru wafadhili na wasamaria wema kwa kuwaunga mkono watoto hao, kwa kuonyesha upendo na kuwakaribisha kwa mikono mikunjufu, akisisitiza upendo wao umewaangazia maisha yao, na wamekuwa msaada muhimu katika kufanya kesho yao iwe yenye nuru.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# TRA yawatangazia neema wakulima

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetangaza neema kwenye sekta ya kilimo nchini, kutokana na kuondolewa misamaha ya kodi katika eneo la kuagiza matrekta nje ya nchi lengo likiwa ni kusaidia kilimo nchini.

Mpango huo wa TRA umetangazwa wakati wa maonesho ya kimataifa ya wakulima, wafugaji na wavuvi yanayoendelea kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa maonesho hayo, Ofisa wa TRA, Mkoa wa Mbeya Nicodemus Massawe, alisema waagizaji wameshaanza kunufaika na msamaha huo wa kodi na kuwataka wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

Massawe alifafanua kuwa fursa hiyo imetolewa kwa matrekta, vitalu nyumba, mbolea na pembejeo zinazohusu kilimo yanapoingia nchini yana msamaha wa kodi kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa.

"Hivi sasa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa waende katika ofisi zetu zote au hapa katika maonesho ya Nanenane, ili wajue ni vitu gani vimesamehewa na gharama zilizosamehewa ni kiasi gani ili anapoagiza hizo zana kwa ajili ya kuboresha kilimo iwe rahisi kwake," alisema Massawe.

Alisema kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato imewekwa katika makundi mawili, mkulima anayelima kibiashara anatakiwa kulipa kodi ya mapato.

Alisema sheria inamtambua mkulima huyo kwa kuangalia thamani ya mavuno yake kama inaanzia Shilingi milioni nne anapaswa kulipa kodi, ikishuka hapo inakuwa ni mkulima wa kilimo cha kujikimu.

Kuhusu vyama vya ushirika alisema vinatakiwa kulipa kodi kulingana na waliyopata kwa mwaka.

"Sheria yetu ya kodi ya mapato imeweka utaratibu kwamba chama chochote cha ushirika ambacho mapato ghafi yake hayazidi milioni 100 kwa mwaka nacho kimesamehewa kodi ya mapato," alisema.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Musibu Shaban alisema wapo Nanenane kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu mamlaka hiyo kwa wananchi.

Alisema kumekuwa na mawazo kwamba mtu akilima kilimo hatozwi kodi lakini ni muda sahihi wa kupata elimu hiyo kutoka TRA.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania-TVLA, Dk. Stella Bitanyi, akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mpemba, Wilaya ya Tunduma, Mkoa wa Songwe waliotembelea banda la TVLA kujifunza kazi mbalimbali za kimaabara zinazofanywa hususani utoaji wa huduma za kiuchunguzi wa magonjwa ya wanyama, uzalishaji wa chanjo za wanyama kwenye maonyesho ya Kimataifa ya Nanenane yanayoendelea katika Uwanja wa John Mwakangale mkoani Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tume yataja kinachokwaza wananchi kuandika wosia

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imesema migogoro ya kugombea mali kwa familia inajitokeza kwa kiwango kikubwa nchini kutokana na wazazi wengi kukataa kuandika wosia kwa hofu kwamba kufanya hivyo watakuwa wanajichulia kifo.

Wakili wa Serikali kutoka katika tume hiyo, Ismail Hatibu, akizungumza na wananchi jana waliotembelea banda kwenye maonesho ya wakulima na wafugaji Nanenane yanayofanyika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, alisema familia nyingi hususani wajane na watoto wamekuwa wakikabiliana na migogoro ya kugombea mali zilizoachwa na marehemu.

"Wajane wengi wanakabiliwa na migogoro kutoka kwa ndugu pindi mume anapofariki, hivyo ni rai yangu kwa watanzania na hasa wanaume kuandika wosia ili kuepusha matatizo yanayoweza kujitokeza kwa mjane na watoto," alisema.

Hatibu alisema, suala la kuandika wosia ni jambo ambalo lipo kisheria, hivyo mzazi anapofanya hivyo anawasaidia watoto na mjane ili wasije kupata changamoto ya kunyang'anyana mali pindi baba yao anapofariki dunia, hali ambayo inaweza kusababisha ugomvi na kukosekana amani ndani ya familia.

"Suala la kuandika wosia ni la kisheria, hivyo wazazi wasiogope kuandika. Ni imani potofu kwamba unapoandika wosia unajichulia kifo. Wosia unasaidia kuepusha migogoro kwa wajane na watoto," alisema.

Ofisa huyo alisema kuwa katika mikoa mingi wanayopita kutoa elimu ya sheria kwa umma, migogoro mingi ambayo inawakabili wananchi ni ardhi, ndoa na mirathi ambayo kutokana na wananchi wengi kutofahanu sheria wamekuwa wakikosa haki zao.

Hatibu alisema baadhi ya faida za kuandika wosia ni kuepusha watoto, mke au mume kunyang'anywa mali, inawezesha kumchagua msimamizi wa miradi, inaepusha migongano katika familia, ndugu au jamaa, inatoa uhakika wa maisha bora ya baadaye kwa warithi kulingana na mali zilizopo na pia inapunguza gharama na usumbufu wakati wa kusimamia mirathi.

Kwa mujibu wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Idhamini (RITA) gharama za kuandika wosia inategemeana na thamani ya mali anazomiliki mhusika, mfano mwenye thamani ya mali ya Sh. milioni 200 kuandika wosia ni Sh. 20,000, mwenye mali kuanzia Sh. milioni 201 hadi Sh. milioni 500 gharama za kuandika wosia ni Sh. 30,000 wakati mwenye mali kuanzia Sh. milioni 501 na kuendelea gharama ni Sh. 50,000.

# Huduma za NSSF mtandaoni zawafurahisha wanachama

**Na Mwandishi Wetu**

UPATIKANAJI wa huduma na taarifa mbalimbali za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kupitia mifumo ya kidijitali umewarahisishia wanachama wake kupata taarifa zao mbalimbali popote walipo bila ya kulazimika kufika katika ofisi za mfuko huo.

Mwanachama wa NSSF, Mussa Malubalo, alisema ameridhishwa na maboresho yanayofanywa hasa ya upatikanaji wa huduma kupitia mifumo ya kidijitali ambayo inarahisisha upatikanaji wa huduma kiurahisi zaidi. Kupitia mifumo hiyo, mwanachama anaweza kuona taarifa zake za michango popote alipo.

Alitoa ushuhuda huo alipotembelea banda la NSSF katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

"Ninawapongeza NSSF kwa kuweka mifumo ya kidijitali ambayo inatusaidia wanachama kupata huduma mbalimbali hasa taarifa za michango yetu na nyingine zinazotuhusu wanachama, nimekuwa nikijaribu kuvuta picha kama NSSF isingeweka mifumo hii ya kidijitali hali ingekuwaje katika kupata huduma, nahisi kwenye ofisi zao zingekuwa zinajaa watu kila siku kwa sababu ya umuhimu wa huduma za NSSF kwa kila mmoja wetu," alisema Mussa.

Pia, alisema kuwa ni muhimu kwa wafanyakazi wa sekta binafsi ambao pia ni wanachama wa NSSF kuhakikisha wanajiunga na mifumo mbalimbali ya NSSF ili kupata taarifa zao kiganjani.

NSSF inashiriki maonesho hayo kwa lengo la kutoa elimu ya hifadhi ya jamii, kusajili wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, elimu kuhusu huduma za NSSF kidijitali, elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, uwekezaji na elimu kuhusu mafao yanayotolewa na NSSF.

**Ninawapongeza NSSF kwa kuweka mifumo ya kidijitali ambayo inatusaidia wanachama kupata huduma mbalimbali hasa taarifa za michango yetu na nyingine zinazotuhusu wanachama.**





# Benki ya Mwanga Hakika yapata faida ya bil.4.06/-

**Na Mwandishi Wetu,** KILIMANJARO

BENKI ya Mwanga Hakika Limited imepata faida ya Sh. bilioni 4.06 kabla ya kodi kwa mwaka ulioishia Desemba 2022, ikilinganishwa na faida ya Sh. milioni 871.78 mwaka wa 2021.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala wa benki hiyo, Hussein Chomete, wakati akisoma taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, kwenye mkutano mkuu wa tatu wa wanahisa, uliofanyika Mwanga mkoani Kilimanjaro, mwishoni mwa wiki.

"Ongezeko hili la faida ni sawa na asilimia 365, ambapo ukuaji huu umesababishwa na ongezeko la biashara ya benki yetu ya Mwanga Hakika uliosababisha kukua kwa amana za wateja," alisema.

Chomete alisema kuwa amana za benki hiyo ziliongezeka kwa asilimia 52 kutoka Sh. bilioni 52.72 mwaka wa 2021 na kufikia Sh. bilioni 86.06.

"Mtaji halisi wa benki pia uliongezeka kutoka Sh. bilioni 16.03 mwaka 2021 na kufikia Sh. bilioni 17.11 kwa mwaka wa 2022; mafanikio haya yametokana na wanahisa kuongeza hisa zao," alisema.

Aidha, alisema thamani ya mikopo iliyotolewa iliongezeka kutoka Sh. bilioni 48.55 mwaka wa 2021 na kufikia Sh. bilioni 80.69 kwa mwaka wa 2022, jambo ambalo alisema limetokana na ukuaji wa kitabu cha mikopo kwa wateja kwa mwaka 2022.

Chomete alisema kuwa Bodi ya Wakurugenzi imeendelea na mipango itakayohakikisha wanahisa wanapata faida na kutoa gawio kwa wanahisa wake ambapo alisema hiyo ni sehemu ya dira ya benki hiyo.

Katika taarifa yake, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Jaghjit Singh, alisema benki imeendelea na mpango mkakati wa 2021-2025 ulioandaliwa na taasisi hiyo kwa kuweka msisitizo katika kuboresha huduma za wateja na kupanua wigo wa biashara.

"Katika mkakati huo mpya, benki inaendelea kujikita katika kuimarisha mifumo mbalimbali ya kiteknolojia na kidijitali ili kuweza kuwafikia wateja wengi zaidi na kutoa ushindani katika soko la ndani na baadaye la kimataifa,"alisema.

Singh aliendelea kusema kuwa faida ya benki hiyo inatarajiwa kuongezeka na kufikia Sh. bilioni 9 kwa mwaka wa 2023 na kwamba mweleкео ni mzuri kutokana na ukweli kuwa hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, tayari faida kabla ya kodi ilifikia Sh. bilioni 4.24.

"Katika kipindi hicho tunatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 127.40 kutoka mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 80.69 iliyotolewa mwaka wa 2022 na hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, tayari tulishatoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 102.81," alisema.

Alisema amana za benki hiyo zinatarajiwa kuongezeka na kufikia Sh.bilioni 132 ikilinganishwa na thamani ya Sh. bilioni 80 zilizokuweko hadi kufikia Desemba mwaka 2022.

"Kwa mwaka wa 2023, benki imeendelea kuimarisha mtaji wake kupitia faida, kwa kuendelea kufanya biashara zaidi na kuendelea kukidhi vigezo vya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambapo kufikia Juni, 2023, mtaji wa benki kisheria ulikuwa ni Sh. bilioni 22.18 hii ikiwa ni juu ya ukomo wa chini wa Benki kuu wa mtaji wa Sh. bilioni 15 kwa benki ya kibiashara," alisema.

Naye Mwenyekiti wa MHB, Mhandisi Rithuan Mringo, alisema malengo ya baadaye ya benki hiyo ni kuhakikisha inakuwa moja ya benki tano muhimu hapa nchini ndani ya kipindi cha miaka 10 ijayo.

Alisema; "katika kuhakikisha tunafikia azma hiyo, bodi na menejimenti ya benki imeendelea kuboresha huduma mbalimbali chini ya kauli mbiu mpya ya benki isemayo Tunatafsiri kesho yako leo," alisema na kuongeza.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akimsikiliza Katibu Tawala, Karolina Mthapula (kulia), alipokagua miradi itakayopitiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru, kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Anna Mbogo. **PICHA: GIFT THADEY**

## Kiwango cha udumavu chapungua Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

OFISA lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi amesema kwa miaka 18 mkoa huo umepunguza hali ya udumavu kwa asilimia 7.6 ambao ulikuwa ukiwaathiri watoto chini ya miaka mitano na kuendelea.

Akizungumza kwenye kikao cha tathmini ya mkataba wa lishe wa mwaka 2022/2023 mkoani Manyara, Dalushi alisema udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 39.6 mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 32 mwaka 2022.

Alisema mwaka 2004 hali ya udumavu mkoa huo ulikuwa asilimia 39.6, mwaka 2010 ukawa 45.8, mwaka 2015 ukawa asilimia 36, mwaka 2018 asilimia 36 na mwaka 2022 udumavu ukashuka hadi 32.

Aliyataja mafanikio ambayo wameyapata kuwa ni kuongezeka kwa usimamizi wa masuala ya lishe katika ngazi zote, kuongezeka kwa mwitikio wa wananchi katika masuala ya lishe, kupunguza udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia 36 hadi 32.

Alitaja mengine ni kuongezeka kwa matumizi ya fedha za kutoka asilimia 51 ambapo ilitolewa Sh. 556 kwa kila mtoto mwaka 2021-2022 hadi asilimia 77.59 ilitolewa Sh. 1072.11 kwa kila mtoto chini ya miaka mitano kwa mwaka 2022/2023.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii mkoani Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema uelewa wa lishe umeongezeka na wanataka uelewa uendelee kuwa mkubwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema ni vizuri mbinu ambazo zinatumika kutokomeza udumavu kama hazifai wataalamu walete mbinu ambazo zinafaa ila kurahisisha upimashishaji wa kudhibiti udumavu kwa watoto.

Akitoa taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Beatrice Lutanjuka alisema udumavu bado uko asilimia 32 kwa watoto chini ya miaka mitano, uzito asilimia 18 na ukondefu asilimia 14.7.

# Madiwani watakiwa kuwa macho ukusanyaji mapato

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Edmund Rutaraka, amewapa 'mtihani' madiwani na watendaji wa wilaya hiyo wa kuwa na jicho la tatu katika makusanyo ya mapato ya ndani yanayokusanywa na wazabuni waliokasimishwa kazi hiyo.

Aidha, amewapa angalizo, akiwataka wasiwaachie pumzi wazabuni hao kupata nafasi ya kupenyeza pembeni pesa za mapato hayo ili kujinufaisha binafsi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha robo ya nne cha Baraza la Madiwani, alisema uamuzi wa kuwapa kazi hiyo wazabuni, badala ya vijana waliokuwa wakikusanya mapato hayo awali, unalenga kuongezeka mapato ya halmashauri hiyo, baada ya kuonekana waliopewa dhamana hiyo wameshindwa na kukusanya fedha.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, njia hiyo ya kuwatumia wazabuni kukusanya mapato itaongeza mapato na kufikia lengo lilikusudiwa.

"Sisi tumeona wale vijana ambao walikuwa wanafanya kazi kama vibarua ya kukusanya mapato, walikuwa hawatumii mashine za POS (mashine za kielektroniki) walizopewa na halmashauri. "Tumefutilia tukaona pesa tunayokusanya ni ndogo na tukaamua kuanzia sasa kuweka wazabuni.

Tumefanya hivyo kwa sababu kipindi cha nyuma, tuliunda timu ya wataalamu kufanya tathmini kwa vipindi tofauti sehemu yenye miradi mikubwa.

...Mfano, chanzo cha chemchemu ya maji moto ya chemka, tulipeleka wataalamu kwa nyakati tofauti na kuna wakati tuliacha kupeleka timu ya uangalizi.

Kwa hiyo tuliona tunapokuwa na timu za uangalizi, mapato yanaongezeka na ndiyo tukaona sasa watu wazabuni watusaidie kukusanya tuweze kufikia lengo tulililoiweka."

Alisema moja ya mambo yaliyowasukuma Hai kufuta vibarua hao kazi na kuwapa jeuri hiyo wazabuni, ni pamoja na vijana kuwa na uwezo wa kukusanya Sh. milioni 230 katika chanzo hicho wakati mzabuni ameingia makubaliano ya kukusanya Sh. milioni 360.

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmshauri hiyo, Dionis Myinga, alisema watashirikiana kwa pamoja kusimamia ukusanyaji wa mapato hayo ili pesa hizo ziende kutekeleza miradi ya wananchi na kutoa huduma muhimu za jamii kama afya na elimu.





# Mil. 40/- zatengwa kukamilisha soko la Ndala lililotelekezwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI imetenga Sh.milioni 40 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Soko la Ndala Manispaa ya Shinyanga, ambalo lilitelekezwa na wafanyabiashara baada ya ujenzi wake kushindwa kukamilika.

**Soko hilo limetelekezwa na wafanyabiashara zaidi ya miaka 10 sasa, kutokana na ujenzi wake kutokukamilika vizuri.**

Fedha hiyo imetengwa na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 lengo likiwa ni kukamilisha soko hilo ili lianze kutumiwa na wafanyabiashara kuwahudumia wananchi.

Akieleza juu ya ujenzi wa soko hilo juzi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwatoa wasiwasi wafanyabiashara hao na kueleza kuwa soko hilo litakamilika kwa wakati ili waanze kulitumia katika shughuli zao.

"Muda si mrefu soko hili litaanza kutoa huduma ya kuuza bidhaa mbalimbali zikiwamo mboga, matunda na wafanyabiashara wajiingizie kipato pamoja na wananchi wasogezewe huduma za muhimu karibu hata ikiwezekana wapate lishe bora," alisema Mndeme.

Awali Diwani wa Ndala Manispaa ya Shinyanga, Zamda Shabani, aliwasilisha kilio chake kwa Mkuu huyo wa Mkoa, kwamba soko hilo limetelekezwa na wafanyabiashara zaidi ya miaka 10 sasa, kutokana na ujenzi wake kutokukamilika vizuri.

Nao baadhi ya kinamama ambao wanauza mboga katika soko hilo, walisema eneo kubwa ni magofu ya majengo na wao hufanya biashara hivyo hivyo, huku wakihofia usalama wao ikiwamo kukabwa na vibaka na kuiomba serikali ikamilishe kujenga.




Shekhe wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Omary Damka (kushoto), akimkabidhi Azan Saidi (kulia), hati ya shukrani ya kutambua mchango wake katika shughuli mbalimbali za kidini, wakati wa maadhimisho ya mwaka mpya wa Kiislamu wa 1,445 uliombatana na uchangiaji wa damu uliofanyika katika Msikiti wa Ijumaa juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# EWURA yawaita wawekezaji kujenga vituo vya mafuta vijijini

**Na Neema Emmanuel,**

MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji Nchini (EWURA) imewataka wawekezaji wanaohitaji kujenga vituo vya mafuta kwenda maeneo ya vijijini ili kusaidia kuondoa majanga ya moto yanayosababishwa na wananchi wanaouza na kuhifadhi mafuta kwenye madumu.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa EWURA, Kanda ya Ziwa, George Mhina, wakati akizungumza na baadhi ya watu waliofika katika banda lao kwenye maonyesho ya wakulima Kanda ya Ziwa Magharibi.

Alisema upatikanaji wa nishati hasa ya mafuta vijijini ni muhimu, hivyo EWURA na serikali wanampango wa kurahisisha upatikanaji wake ili kuwaondolea adha wananchi ya kuhifadhi mafuta kwenye madumu ambayo kuna wakati yanapoteza ubora na kuwa hatarishi katika mazingira.

Alieleza kuwa tayari wamekuja na kanuni ambazo ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini umerahisishwa, hivyo wafanyabiashara wachangamkie fursa hiyo kwa sababu EWURA imepunguza masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini kulinganisha na mijini.

"Kijijini hatuhitaji hati ya ujenzi kutoka halmashauri, kibali kutoka NEMC, masharti ya urefu wa paa tumeondoa bali tutahitaji tu barua ya mkurugenzi ioneshe kuwa kituo hicho hakitakuwa na madhara kwa mazingira na ujenzi wake ni wa kawaida, lengo ni kuhamasisha ujenzi wa vituo hivi vijijini," alieleza Mhina.

Anaeleza kuwa serikali katika kuunga jitihada za EWURA kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imetenga bajeti kwa mwaka wa fedha ulioisha na wa sasa ambapo inakusudia kukopesha wananchi kuweza kumudu vigezo na masharti vilivyo ainishwa kwenye muongozo, ambapo anaweza kukopeshwa mtanzania hadi Sh. milioni 50 na ukajenga kituo cha mafuta kijijini.

Kuhusu nishati ya umeme, Mhina alisema majanga ya moto yamekuwa yakiongezeka mara kwa mara, kuwataka mafundi waliohitimu mafunzo ya umeme kuhakikisha wanafika EWURA ili kupata leseni na kutambulika kisheria ili kusaidia wananchi wanaotumia vishoka kuunganishiwa umeme kupata huduma hiyo kwa urahisi.

## Bwawa la maji kunufaisha vijiji nane mkoani Shinyanga

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI zaidi ya 30,800 kutoka vijiji nane katika Kata ya Isagehe Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wanatarajia kunufaika na mradi wa bwawa la maji linalojengwa na halmashauri kwa ushirikiano na mgodi wa Barrick Buzwagi.

Bwawa hilo lenye la Sh. bilioni 2.8 linajengwa katika vijiji vya Malenge, Bukooba, Isagehe, Lunyashi, Mpera, Sungamile, Mwalemo pamoja na Mwakata ambako idadi kubwa ya wananchi wake wanategemea kilimo kwa asilimia 95 kulinganisha na vijiji vingine vyenye madini.

Diwani wa Isagehe Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Maganga Thomasi, aliyasema hayo hivi karibuni katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi uliofanyika Kijiji cha Lunyashi-Isagehe.

Alisema mradi huo unatarajia kukamilika Aprili, 2024 na wananchi wataanza kunufaika kupitia kilimo cha umwagiliaji na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuacha kabisa kuendelea kutegemea mvua ambazo zimekuwa zikinyesha kwa kusuasua kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Thomasi alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 230 zimetumika katika ujenzi wa ghara la kuhifadhi chakula ambacho kitakuwa kimepatikana na ununuzi wa mashine ya kisasa ya kukoboa na kulipa ubora mpunga ambao utakuwa ukipatikana kupitia kilimo na watahakikisha wanautunza ili uzidi kuwanufaisha.

Mkazi wa Kijiji cha Mpera, Sarah Masanja, alisema msimu huu wamepata mavuno kidogo kutokana na kutokuwapo kwa mvua ya uhakika na mazao waliyoyapata ni kwa ajili ya chakula cha familia, hivyo kutakapokamilika kwa mradi huo watazalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na kujiingizia kipato cha kaya.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, alisema serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeendelea kuboresha sekta ya kilimo, hivyo mradi utakapokamilika wahakikishe wanautunza ili uzidi kuwanufaisha kwa pamoja na wale watakaobainika kuhujumu mradi huo wawalipoti kwa ajili ya kuwachukulia hatua.

Aidha, Kishimba aliwataka vijana kuchangamkia fursa ya pembejeo za kilimo ambazo zimekuwa zikitolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa vijana wenye uwezo wa kulima hekari tano na kuendeleza mazao ya chakula na biashara, kwani mazao yanayopatikana ni mali yao na siyo ya halmashauri.

Nipashe
# NANE NANE 2023
Jumanne Agosti 8, 2023

"VIJANA NA WANAWAKE NI MSINGI IMARA WA MFUMO ENDELEVU WA CHAKULA"





Ukurasa 12

TARI 'inavyomtoa' mkulima shambani, ikitekeleza agizo la Rais kunusuru ngano

AFRO WORLD AGRI FOOD 2023

*This time to Africa...*

Ukurasa 13

Baada ya kuwasherehekea wakulima sasa ni kongamano kimataifa la chakula

ELIMU

NA PETER ORWA

# Ubunifu kilimo Awamu ya Sita katika staili kuendeleza yake Baba wa Taifa

WAKATI unapatikana uhuru wa nchi, moja ya mbinu mkakati wa maendeleo ililenga sekta ya kilimo, kuanzia kwenye falsafa ya umma, sera na mfumo wa uchumi kitaifa.

Ikirejewa maana ya maendeleo kupitia tafsiri ya kitafiti ya mwanazuoni Profesa Walter Rodney, mwenye historia ya kushika chaki, pia kuandika vitabu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anaitafsiri maendeleo kuwa ni mabadiliko ya kusonga kwenye idadi na ubora wa vitu vinayoandaliwa au kuzalishwa.

Katika mikakati yake kihistoria, mwasisi wa taifa Mwalimu Julius Nyerere, akaiweka sekta kilimo katika mikondo tofauti, ikiwamo kuzamisha elimu kwa wakulima.

Ikianzia na hotuba yake kihistoria, hadi matendo na hususani Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Nchi, 1964 - 1969 ambayo kimsingi ni dira ya taifa hadi sasa, kilimo kimeshika nafasi yake kitaifa ikiwa 'sekta mama' mkuu huyo wa nchi akiwajibika katika matamshi ya hotuba kila mara akisistiza 'mpunga (umbali) tunapanda nchi moja moja...'

Hata baadaye mwaka 1967, kwenye utekelezaji wa Azimio la Arusha, kupitia matamshi na maandiko yake mbalimbali kama vile nadharia ya 'Elimu ya Kujitegema' na maudhui ya vitabu kama cha Ujamaa, nafasi ya upeo katika kuwa na kilimo bora kwa mkulima ikashuhudiwa.

Elimu ya Kujitegemea, nadharia aliyohimzia zaidi Mwalimu Nyerere ililenga kumboresha msomi wa Kitanzania, kuanzia elimu ya msingi ambayo imebaki kuwa ya lazima, hata chini ya hapo kwa ambao hawakuipata, wakinufaishwa kwenye 'kisomo chenye manufaa.'



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua mazao ya kazi za shambani. Anayempa taarifa ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MTANDAO.**

Inapoangaliwa kwa kina, mkulima amekuwa na nafasi kubwa ikizingatiwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wakati huo walikuwa wakulima na kwa maana hiyo. Hapo inamaanisha ni elimu kwa mkulima, kukidhi maisha yake nyumbani na ya shambani.

Hadi sasa Elimu ya Kujitegemea imebaki kuwa tawi kubwa ya elimu kitaifa, ikitiliwa maanani ni sehemu ya Sera ya Elimu ya sasa na kilimo kikiendelea kushika nafasi kubwa ya uchumi, huku serikali iliyoko madarakani chini ya Rais. Dk, Samia Suluhu Hassan, ikiweka mkakati kukifanya kuwa mwajiri mkuu kitaifa.

Kwa mujibu wa malengo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), wana mtazamo mkubwa katika kundi la kinamama na vijana, ambao ndio jeshi kubwa kitaifa.

Tayari Mwalimu Nyerere, tangu anaasisi uhuru wa nchi alishaweka mkazo kwa majukumu ya TARI, akizipanua na kuyapa malengo mapya, kukidhi mahitaji ya kitaifa, kutoka kwenye yale ya kikoloni.

Kwa upande wa ubunifu wa elimu ya juu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akakipatia tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo Morogoro (sasa SUA), ambacho hadi leo ni mbia mkubwa wa TARI.

**AWAMU YA SITA**

Kadri inavyoangaliwa mikakati, falsafa, sera, hadi malengo ya sekta za kilimo na mifugo nchini, daima inasimama katika mstari mmoja na ubunifu wa Mwalimu Nyerere, hasa kuanzia mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano nchini wa mwaka 1964 hadi 1969, iliyofuatiwa na nyingine kama hiyo.

Hadi sasa, Rais wa serikali ya Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kipaumbele kikubwa kwa sekta ya kilimo, katika falsafa na kipaumbele kilekile cha mwaka 1964, tofauti ikiwa ni mahitaji ya wakati husika.

Wakati mtazamo uliopita ulilenga kujitosheleza kwa chakula, pia kuepuka hali ya 'kuzalisha tusichokitumia na kutumia tusichozalisha' jibu lake ilikuwa ni kupanua mashamba kuzalisha chakula na malighafi, pia kuwa na viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi hayo; kinachofanyika nchini 'operesheni viwanda.'

Imeshuhudiwa juhudi binafsi za Rais Dk. Samia, pia kiserikali katika sura pana na mikakati akiwekeza nguvu kubuniwa viwanda, sasa kukionekana viwanda vipya vya sukari kumaliza uhaba huo, huku wakala wa kihistoria wa mageuzi ya teknolojia shambani TARI, ikipewa majukumu maalumu.

TARI inawajibika sasa kuhakikisha, ifikapo mwaka 2030, kuwezesha nchi ijitegemee kwa upa-

INAENDELEA UK.12

NA ASHTON BALAIGWA, MBEYA

# TARI ‘inavyomtoa’ mkulima shambani, ikitekeleza agizo la Rais kunusuru ngano

IMEFIKA kilele cha Sikukuu ya Wakulima, iliyozinduliwa na Makamu wa Rais Dk Philip Mpango, ikiwa na maonyesho ya kimataifa ya wakulima, wafugaji na wavuvi katika kiwanja cha John Mwakangale, huku uwanja huo ukitangazwa kuwa wa kudumu.

Kuanzia mwakani inaelezwa itahuwasisha wakulima, wavuvi na wafugaji kutoka nchi zote za Afrika na Watanzania kujifunza.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anasema tayari serikali imeshatenga bajeti ya marekebisho ya miundombinu ili iweze kumudu hadhi ya kimataifa.

Waziri Bashe anasema, wameshakubaliana na mabalozi mbalimbali nchini, kuanzia mwakani 2024, wataalikwa viongozi na wakulima wa nchi zote za Afrika, wakulima na wafugaji wao pamoja na wanunuzi wa mazao wawe na eneo lao kuonyesha teknolojia zao.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeyapokea hayo kwa bashasha kwa kuyaongezea thamani maonyesho hayo kushirikisha nchi nyinginezo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, anasema kupitia vituo vyake mahiri vilivyopo nchi nzima, ni fursa kwao licha ya ukinzani duni kwa teknolojia mpya ya kilimo na mbegu nchini, sasa watafika mbali kimatifa.

Dk Mkamilo anasema TARI katika maonyesho ya wakulima imekuwa ikifikisha matokeo ya tafiti za mbegu za mazao mbalimbali kwa ajili ya tija shambani.

Anasema TARI ina jukumu la kugundua au kuainisha teknolojia kuanzia mbegu na ubunifu wa mbinu za kilimo bora nchini, huku wakiweka nguvu katika mazao ya kimkakati.

Anasema maonyesho hayo ya kilimo mkoani Mbeya na mengine kama hayo kwenye kanda tofauti nchini, TARI imekuja na teknolojia za ugunduzi wa aina za mbegu za aina mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, anasema kupeleka timu ya watafiti katika maonyesho hayo ya wakulima,wafugaji na wavuvi yanayofanyika katika kanda tofauti nchini, inalenga kuhakikisha wakulima na jamii wanapata elimu ya kutosha kuhusu teknolojia hizo.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, (TARI) Dk Geofrey Mkamilo (kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendogo, kwenye maonyesho ya Nanenane, jijini Mbeya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

“Sisi hatuishii kufanya utafiti tu lakini tunahakikisha hizi teknolojia tunazozivumbua zinawafikia wakulima,” anasema na kutaja majukumu yao mengine ni kufikisha teknolojia sahihi kwa wakulima, wakishirikiana na halmashauri mbalimbali nchini, pia vyombo vya habari.

Dk. Mkamilo anafafanua, TARI imeanzisha vituo vya kutoa mafunzo kwa wakulima kujifunza teknolojia za kisasa na kuunganishwa katika mnyororo wa thamani kwa vituo hivyo vinavyotoa elimu.

Anasema, vituo hivyo vinalenga kusogeza huduma za kitaalamu, kuepuka kilimo cha mazoea. Kwa mujibu wa Dk Mkamilo, TARI ina jumla ya vituo 17 vya utafiti nchini na zipo kwenye biashara na uwekezaji na mnyororo wa thamani kwa kuwa wapo wanaowekeza kilimo, usindikaji na wanawekeza kufanya biashara.

Anasema kwa sasa kipaumbele kikubwa kipo kwa vijana na kinamama kuendeleza kilimo

**TEKNOLOJIA ZA TARI**

Mkurugenzi Mkuu wa TARI. Anasema katika maonyesho hayo, wameleta teknolojia nyingi.

Pia, Mkurugenzi wa kituo cha TARI Mlingano, Tanga, Dk Catherine Senkoro, anasema katika maonyesho hayo, wakulima wanajifunza matumizi ya udongo kulingana na mazao wanayokusudia kulima katika maeneo yao, ikiwamo fursa ya kupimwa kwa udongo.

“Tunawafundisha wakulima umuhimu wa afya ya udongo kwenye maonyesho haya ili kuwasaidia wakulima na kuwashauri kabla ya kuamua kufanya kilimo cha mazao mbalimbali ni vyema wakapima udongo wa shamba husika ili kujua na kupata ushauri nini cha kufanya ili kupata tija katika kilimo” anasema Dk Senkoro.

Mratibu wa Programu ya Ufuta Kitaifa kutoka TARI, Naliendele Mtwara, Joseph Nzunda, anasema utafii umeonyesha magonjwa ya fangasi na bakteria, yameweza kupatiwa ufumbuzi kwa kupitia zao la ufuta

Anasema, katika utafiti imebainika kuwa zao hilo limeweza kuongezwa thamani na kutengenezea mafuta ya kujipaka ambayo yanamaliza tatizo hilo la fangasi na bakteria.

Nzunda anataja umuhimu wa mafuta ya ufuta, kuna kemikali na virutubisho mbalimbali pamoja na vitamini E.

“Bidhaa hiyo inatumika katika kutunza ngozi kwa sababu ndani ya ufuta kuna kemikali mbalimbali” anatamka na kuendelea:

“Mafuta haya yanaitwa Sesalemo yanatokana na ufuta pamoja na kwamba yana mchanganyiko wa vitu vingine. lakini asilimia 90 zaidi inakua ni ufuta.”

Anasema mbali na mafuta hayo, zao hilo linatumika kutengeneza bidhaa nyingine kama mafuta ya kupikia, mashudu ya mifugo kama kuku, mbuzi na wengineo.

Mtafiti Nzunda anasema, katika zao la ufuta linatumika kuzalisha vyakula kama kashata, unga na siagi.

**OPERESHENI NGANO**

Mtafiti Mwandamizi wa zao la ngano nchini kutoka kituo cha TARI mkoani Arusha, Ismail Ngolinda, anasema kwenye maonyesho, wakulima wanapewa mbinu za uzalishaji wa zao hilo, inayoendana na mkakati wa serikali, ili kukidhi mahitaji ya nchi na kuacha kuagiza kutoka nje.

Anasema kwa sasa mahitaji ya ngano ni tani milioni moja kila mwaka huku uzalishaji wake ukiwa ni tani 100,000 pekee kwa mwaka, ikiacha pengo la tani 900,000.

Mtafiti Ngolinda, anasema serikali imeipa jukumu TARI, kuongeza uzalishaji wa mbegu za zao la ngano na kupanua mashamba mengine mapya.

Ngolinda anasema, tayari wameanza mkakati ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, Tanzania inajitegemea kwa kuzalisha zao hilo kukidhi mahitaji ya ndani, ikianzia na mbegu za awali na teknolojia ya kisasa inayohimili ukame.

Anasema kupitia mkakati huo, TARI itazalisha mbegu za awali tani 2500 zitakazozalisha tani 50,000 za mbegu zilizothibitishwa ubora ambazo zitaweza kupanda eneo la hekta 400,000 ambazo zitaweza kuzalisha zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka na kukidhi mahitaji ya ngano hapa nchini na ziada kuuza nje.

Mtafiti huyo anasema tayari uzalishaji wa mbegu hizo za awali umeshaanza kwenye mashamba ya TARI yaliyopo katika vituo vyake vya Silian (Arusha) na Uyole (Mbeya) na Kifililo mkoani Iringa ambapo katika kipindi cha mwaka jana zilizalishwa tani 50 na mwaka huu tayari zimezalishwa tani 250 huku mikakati ya uzalishaji zaidi ikiendelea.

Anasema katika kutekeleza maagizo ya serikali, wanakusudia kuongeza maeneo ya uzalishaji wa kilimo hicho cha ngano kwenye mashamba mapya yaliyopo katika mikoa ya Tanga, Kigoma, Ruvuma, Geita na Morogoro.

Ngolinda ambaye ni mratibu wa zao hilo la ngano kitaifa, anataja maeneo mengine mapya ambayo yana sifa ya joto na mvua chache yatakayolimwa zao hilo la ngano baada ya kukamilika kwa utafiti wa mbegu zake zitakazopasishwa kwaajili ya kuhimili hali hiyo ni pamoja na mikoa ya Dodoma,Singida na Tabora.

**SAUTI YA MKULIMA**

Mariam Masige, mkazi wa jijini Mbeya, anaiambia Nipashe katika maonyesho hayo kwenye banda la TARI, akiunga mkono kuvutiwa na mafuta ya ufuta kwa kumaliza tatizo la ngozi lililomsumbua sana mwaka jana.

## UBUNIFU KILIMO AWAMU YA SITA KATIKA STAILI KUENDELEZA YAKE BABA WA TAIFA

**INATOKA UK.11**

tikanaji ngano, vilevile tayari matunda yakionekana kwa upatikanaji mafuta ya kupikia nchini.

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, uwekezaji upo njiani kuwezesha uchakataji matunda kwa wingi nchini na ziara zake amekuwa akioanisha na kukaribisha uwekezaji katika sekta ya kilimo kitaifa.

Ndani ya miaka miwili iliyopita ya uongozi wa Dk. Samia, kumeshuhudiwa tena aina ya vipaumbele vya Mwalimu Nyerere, kupitia kupanuka bajeti ya kilimo maradufu inayokaribisha vipaumbele vya kilimo cha kisasa, ikiwamo umwagiliaji.

Kingine kinachoweka historia kimataifa, ni kuanzishwa kituo cha kilimo cha kisasa na kujitegemea kwa vijana, huko Bahi, Dodoma, ikiwa kwenye msingi wa ‘Elimu ya Kujitegemea’ kikiwakomboa vijana na tatizo la ajira, ambalo wameanza na kundi la vijana 300 wa mfano.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Baada ya kuwasherehekea wakulima sasa ni Kongamano Kimataifa la Chakula

•Kampuni 700 zatua Dar, Watanzania waambiwa 'hakuna kulala, wajitokeze'




WAKATI leo ni kilele cha Nanenane, wafanyabiashara na wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali wanawapa tena Watanzania fursa ya kushiriki kongamano na maonyesho ya kimataifa ya mazao ya chakula-'Afro Agri World Food 2023'.

Ni jukwaa linalowaleta pamoja wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wa kilimo kutoka Afrika, Asia, Ulaya na Marekani wanaokusanyika Diamond Jubilee, kuanzia Alhamisi Agosti 10 hadi 12, jijini Dar es Salaam kujionea mazao mbalimbali ya chakula, kusaka masoko, utaalamu na ujuzi.

Ni zaidi ya washiriki 700 watakuwa nchini kwa siku tatu kuhudhuria kongamano na maonyesho ya kimataifa ya 'Afro World Agri Food 2023', anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tanzania Pulses Network (TPN), Zirack Andrew, moja ya kampuni waandaaji.

Anasema mazao yatakayoonyeshwa ni pamoja na ya viungo, mbegu za mafuta kama korosho na ufuta, yapo matunda, sukari, ngano, pamba, kokoa, kahawa, chai, mchele na nafaka mbalimbali, mikunde kuanzia mbaazi, maharage, kunde, dengu, njegere na njugumawe.

**MALENGO YA MAONYESHO**

"Ni kuhamasisha uwekezaji wa kimataifa kwenye sekta ya kilimo Afrika, kutengeneza fursa za kibiashara kwa wafanyabiashara, kuwa jukwaa la majadiliano kwenye mazao tofauti Afrika na kutoa fursa ya kuonyesha teknolojia zinazotumika kwenye sekta ya kilimo Afrika," anasema Andrew.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Pulses Network, anasema kongamano hilo linafanyika kwa mara ya kwanza Afrika na Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wake, alisema litakuwa na mambo kadhaa ambayo ni pamoja na maonyesho ya bidhaa za chakula na midahalo ya mazao tofauti ya chakula yanayozalishwa Afrika.

Aidha, kutoa tuzo kwa kampuni mbalimbali kwa lengo la kutambua mchango wao mahusus kwenye kuendeleza mazao na biashara ya chakula Afrika na na mikutano ya kuzungumzia biashara na kuingia mikataba na makubaliano ya kibiashara.

"Kongamano hili limeandaliwa na Vyama vya Mazao Afrika, Tanzania Pulses Network (TPN) kwa kushirikiana na kampuni ya Taso Event Private Limited ya India ambayo imekuwa ikiandaa majukwaa kama haya takribani miaka 20 huko India, Mashariki ya Kati na nchi ya Myanmar." Anasema Andrew.

Anaeleza kuwa mazao yatakayohusika na jukwaa hilo na kujadiliwa wakati wa kongamano ni viungo, korosho, sukari, ufuta, ngano, pamba, kokoa, kahawa, chai, mikunde kama mbaazi, maharage, kunde, dengu, njegere na njugumawe.

Halikadhalika, anaongeza kuwa kongamano hilo limechagua mazao haya kwa sababu ndiyo yanazalishwa kwa wingi Afrika ikiwemo Tanzania na pia yana uhitaji mkubwa katika soko la kimataifa hasa katika nchi za Asia na Ulaya.

Andrew anawaomba Watanzania wanaozalisha mazao hayo kutumia fursa hiyo akiwakaribisha kuonyesha bidhaa zao lakini pia kushiriki kongamano ili kutangaza wanachozalisha na kutafuta masoko kwa nchi washiriki.

Halikadhalika wajionee na vile vinavyozalishwa na kampuni mbalimbali duniani na jinsi ya kushirikiana na wazalishaji wengine wa nje ya mipaka.

"Mtanzania ambaye atakuwa tayari kushiriki au kuonyesha bidhaa zake awasiliane na Tanzania Pulses Network kupitia website yao ya www.tanzaniapulses.co.tz," alisema

Anawataka pia washiriki kongamano na mikutano ya kibiashara, kutembelea mabanda yenye mazao ya kilimo na kuhudhuria mikutano ya kibiashara, akikumbusha kuwa watakaoshiriki kongamano watatakiwa kulipia ada ndogo ya ushiriki.

Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula, nchi ikiwasilishwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2023/2024, anasema kwa msimu wa mwaka 2021/2022 yalifikia tani 17,148,290.

Hata hivyo, kuna upungufu ikilinganishwa na tani 18,665,217 mwaka 2020/2021 ikiwa zimepungua kiasi cha tani 1,516,927, akisema ni kutokana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

Aidha, Waziri Bashe anasema uzalishaji wa nafaka ambao unahusisha mahindi, mchele, mtama uwele, ulezi na ngano ulipungua kwa tani 1,641,127 sawa na asilimia 15.1 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 10,874,425 kwa msimu wa 2020/2021.

Akizungumzia uzalishaji wa mazao yasiyo nafaka ambayo ni jamii ya mikunde, muhogo, ndizi, viazi vitamu na mviringo anasema uliongezeka kwa tani 124,200 sawa na ongezeko la asilimia 1.6 na kufikia tani 7,914,992 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 7,990,792 msimu wa 2020/2021.

Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2022/2023 Waziri anasema ni tani 15,053,299 na kuna ziada ya tani 2,095,256 za chakula, kwa kuzingatia takwimu hizo za uzalishaji na mahitaji ya chakula, kwa mwaka 2022/2023, Waziri anasema taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 114.

Kwa upande wa makadirio ya mahitaji ya chakula, Waziri analiambia bunge kuwa hadi ifikapo 2030 mahitaji yatakuwa tani milioni 20 na mwaka 2050 yatafikia tani milioni 33.7.

"Hali hii inaleta changamoto kwa nchi yetu tunawajibika kuwa na mikakati ya uwekezaji ya muda mrefu tena endelevu kwenye sekta ya kilimo ili kuhakikisha utoshelevu wa chakula kwa miaka hiyo na ziada kwa ajili ya kuuza nje." Anasema.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2022 , idadi ya Watanzania ni takribani milioni 61 na mwenendo wa ukuaji wa idadi ya watu nchini na duniani ifikapo mwaka 2050, Tanzania itakuwa na watu milioni 136 na duniani watafikia bilioni 9.7.

Katika kipindi hicho, uzalishaji wa chakula unakadiriwa kupungua kwa asilimia nne wakati mahitaji halisi ya chakula yanakadiriwa kuongezeka kwa zaidi ya asilimia 50.

Changamoto kubwa ya uzalishaji wa chakula namba moja kwa Tanzania inatajwa na Waziri Bashe kuwa ni mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula na hivyo kuhatarisha uimara wa uchumi na usalama wa chakula.

Ili kuwa salama kwenye eneo hili ni lazima kuendelea kuwekeza katika mifumo imara na himilivu ya kilimo inayotumia teknolojia za umwagiliaji za kisasa, uwezo wa kuhifadhi mbegu za asili ili kuwa msingi imara wa kufanya utafiti kupata teknolojia bora za uzalishaji wa mbegu ili kujihakikishia usalama wa chakula na ulinzi wa uchumi wa taifa, anasema Waziri.

NA MWANDISHI WETU

# Balaa la viuatilifu; mkulima anapata maradhi kifafa, usonji, 'pakinsoni'...



Viua wadudu waharibifu na mbolea si salama sana kwa wanadamu na ikolojia **PICHA: MTANDAO**

DAWA za kuua wadudu au viuatilifu hutumiwa karibu duniani kote ili kudhibiti visumbufu vinavyoua mazao mashambani na hata mimea mingine inayomuhusu binadamu.

Ingawa ni dawa zinazofaa, lakini si salama, zina kemikali zenye sumu zinazoweza kuharibu mifumo ya fahamu na neva.

**ATHARI KIAFYA**

Viuatilifu vina madhara, ukila kupitia chakula au mazao yaliyotokana au kukuzwa na kulindwa na dawa hizo.

Athari ni kupitia mchakato unaojulikana kama malimbikizo au mkusanyiko wa kibayolojia (biological accumulation).

Hii hutokea wakati sumu inapoongezeka mwilini kwa sababu hauna uwezo wa kuivunja na kuiondoa.

Kwa hivyo viuatilifu vingi vinaweza kurundikana kwenye mafuta mwilini na kuwa na athari mbaya kwa binadamu.

Licha ya kanuni za kimataifa kuhusu matumizi yake,utafiti unaonyesha kuwa si salama.

Inapopulizwa, dawa za kuulia wadudu huzalisha unaogeuka kuchafua hewa.

Nchini Marekani, asilimia 37 hadi 54 ya magonjwa yanayohusiana na dawa kati ya wafanyakazi wa kilimo yanahusishwa na kuvuta hewa ya dawa.

**DALILI MBAYA**

Dalili za mapema za kuathirika na dawa za kuua wadudu zinaweza kujumuisha maumivu ya kichwa, kichefuchefu, kizunguzungu na mfumo wa upumuaji, anasema Michelle Perro,anapozungumza na BBC.

Ni daktari wa watoto ambaye alianzisha shirika lisilo la kiserikali la GMO Science, jukwaa la umma ambalo madaktari hujadili na kuchambua athari za mazao na vyakula vilivyotengenezwa kwa kubadili vinasaba.

Anataja athari za kiafya kuwa zinaweza kuwa kifafa hadi matatizo ya kupumua. Hali na matumizi ya muda mrefu wa aina ya dawa inayotumiwa pia husababisha athari kwenye mifumo ya hisia na neva.

"Kwa kuvuta viuatilifu kupitia mapafu inaweza kuwa sumu zaidi, kwa sababu utumbo wetu una vijidudu ambavyo husaidia kuondoa sumu," anasema Perro.

Dawa za viatilifu zinaweza kusababisha kupoteza uwezo wa kutambua harufi za vitu mbalimbali.

Utafiti wa mwaka 2020 uligundua kuwa kati ya wafanyakazi wa kilimo wanaokadiriwa kuwa milioni 860 duniani asilimia 44 wanaathiriwa na sumu ya dawa hizi kila mwaka, inasema BBC.

Hii ni kutokana na ukosefu wa vifaa vya kujikinga au kutumia vifaa vyenye kasoro, ambayo husababisha athari kupitia ngozi, kuvuta hewa au kumeza.

"Dawa za kuulia wadudu zinapoingia mwilini kwa kuvuta pumzi, hupitia kizuizi cha ubongo wetu wa damu na kudhoofisha utendakazi wa neva au mishipa ya fahamu," anasema Chen. "Njia nyingine, dawa za kuua wadudu zinaweza kuingia katika mfumo wetu wa damu kupitia njia ya utumbo ikiwa zimemezwa ama kuliwa."

Tafiti nyingi pia huonyesha uhusiano kati ya matumizi ya dawa hizi na magonjwa ya mfumo wa neva.

Dawa za kuulia wadudu zimehusishwa na hali kama vile ugonjwa unaoitwa kitaalamu attention deficit hyperactivity disorder (ADHD).

ADHD inasababisha kutokujiamini, kushindwa masomo shuleni au kazini na dalili zake ni pamoja na kukosa umakini au kuwa nao lakini mdogo na kuhangaika.

Aidha, maradhi ya Parkinson nayo pia husababishwa na dawa hizo , huu

ni ugonjwa wa ubongo ambapo mtu hukosa homoni ya 'dopamine' baada ya seli zinazotengeneza dopamini kuharibika.

Mgonjwa anatetemeka mikono pamoja na shida ya kutembea. Huenda pia mtu akawa na shida za kufikiria.

Dawa za kuua wadudu wakati wa ujauzito au kwa watoto pia zinahusishwa na tatizo la usonji.

Kwa sababu zimetengenezwa kulenga tishu za neva za kiumbe, viua wadudu kama vile 'organofosfati, carbamates na organochlorine' ni hatari zaidi kuliko viua magugu.

Mnamo 2014, watoto wa shule moja waliathirika na sumu hizo huko Bordeaux, Ufaransa, kwenye shule hiyo ya msingi iliyo karibu na shamba la mizabibu, wanafunzi 23 walipata kichefuchefu, maumivu ya kichwa na kuwashwa baada ya dawa za kuua kuvu kunyunyiziwa shambani mizabibu,inasema BBC.

BBC inaripoti kisa cha Tim Parton, meneja wa shamba wa Park huko Staffordshire Uingereza, aliyeanza majaribio ya kilimo cha kibaolojia kisicho na kemikali.

Badala ya kutumia dawa za kuulia wadudu na mbolea, alizigeukia pembejeo asilia.

Kilimo hicho ni mbinu mpya ambayo inatanguliza mbele udongo na afya ya mazingira kwa kupunguza pembejeo za bandia au zenye kemikali.

**SABABU YA KUBADILIKA**

BBC inasema anaanza kulima kibailojia baada ya kuumwa na kichwa na kuota vipele kwenye ngozi kutokana na kutumia viuatilifu vyenye kemikali.

Tangu atumie mbinu ya kilimo cha kibaolojia, Parton hajapata athari zozote za kiafya. Hajalazimika kutumia mbolea yoyote ya fosforasi na potasiamu kwenye mazao yake kwa zaidi ya miaka 10.

"Ninajaribu kuweka mmea katika uwiano wa lishe niwezavyo, na ikiwa mmea umepata lishe sahihi, hauugui," anasema.

**ILIVYO DUNIANI**

Hali ya matumizi ya viuatilifu duniani ni kubwa na hivi ni vitu au kemikali zinazotumika kufukuza, kuharibu na kudhibiti wadudu, magugu au viumbe vingine vinavyoathiri ukuaji wa mimea.

Ingawa ni bora, dawa za kuulia wadudu zina kemikali zenye sumu ambazo zinaweza kuwa na athari kubwa na wakati mwingine ni hatari kwa viungo vya hisia vya binadamu na mfumo wa neva.

BBC inasema kemikali hizo zilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza katika miaka ya 1930 ili kulinda mazao nchini Marekani.

Jumuiya nyingi za kilimo zinategemea matumizi ya dawa au viuatilifu kwa sababu ya kufanikisha kupata mavuno mengi.

Leo, karibu theluthi moja ya bidhaa za kilimo duniani zinategemea dawa hizo zenye kemikali.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuna zaidi ya aina 1,000 za viuatilifu zinatumika duniani kote, huku baadhi ya aina zinazojulikana zaidi ni dawa za kuulia magugu, za kuondoa ukungu na bacteria.

Mnamo 1990, matumizi ya viuatilifu duniani yalikuwa kilo bilioni 1.69; idadi hii ilikua zaidi ya asilimia 57 katika miongo miwili iliyopita, na kufikia kilo bilioni 2.66 mwaka 2020, inasema WHO.

Ripoti ya Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP) inatabiri kuendelea kukua kwa matumizi ya viuatilifu.

Inasema kwa kuwa idadi ya watu duniani inatarajiwa kufikia watu bilioni 9.3 ifikapo mwaka 2050, ongezeko la asilimia 60 la kiwango cha uzalishaji wa chakula linahitajika.

UNEP inaongeza kuwa ili kuendeleza na kukidhi mahitaji haya, watafiti wanaamini wakulima watahitaji kutumia dawa ama viuatilifu vingi ziadi kupambana na wadudu, magugu na magonjwa ya mimea.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa utafiti wa mifumo ya kilimo ya Ulaya, kuacha kutumia dawa za kuua wadudu kunaweza kusababisha hasara ya asilimia 78 ya uzalishaji wa matunda, kupungua kwa mavuno ya mboga kwa asilimia 54 na hasara ya asilimia 32 ya mazao ya nafaka.

Lakini, utegemezi wetu kwa dawa za kuulia wadudu pia huja kwa gharama kubwa kwa mazingira, na utafiti unaoonyesha dawa za kuulia wadudu zinaweza kuwajibika kwa upotezaji wa harufu katika nyuki wa asali, kuchafua vyanzo vya maji, na kutishia mifumo ya ikolojia ya majini.





# Wafugaji kuku walalamika kususwa na wataalam mifugo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFUGAJI wa kuku Kanda ya Kati wamewaomba wataalam wa mifugo kuwatembelea kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuwapatia elimu ili kuboresha ufugaji.

Mkurugenzi wa Taasisi ya kikundi cha Tusumuke Dodoma, Christopher Makotwe alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza katika kongamano la wafugaji wa kuku.

Kikundi hicho kinajishughulisha na usambazaji na uzalishaji wa vifaranga vya kuku, vyakula vya mifugo chanjo na dawa.

Alisema wataalam hao wa mifugo ya kuku wanahitajika kwa wafugaji ili kuwapatia elimu itakayowawezesha kuongeza uzalishaji na kuwainua kiuchumi.

"Wakati umefika sasa wafugaji wa kuku wanahitaji kutengeneza vyakula vya kulisha mifugo inayotokana na ubunifu wao na tumechoka kuagiza vyakula vya nje, hivyo tunawaomba wataalam wa mifugo kututembelea na kutupatia elimu ya ubunifu utakaowawezesha kuibua vyakula kwa kutengeneza wenyewe,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bahi, Donald Mejitii akifungua kongamano hilo aliwataka wataalamu kubuni mbinu itakayoongeza uzalishaji wenye tija badala ya kuendelea kusubiri makongamano.

Alisema kuwa hivi sasa soko la kuku limepanda kwa kasi kwa Kanda ya Kati, hivyo wataalam wanahitajika kuwafikia wafugaji ili kuchangamkia fursa hiyo.

"Hivyo kupitia kongamano hili nitumie nafasi hii pia niwaombe wataalam wetu mliopo kwenye halmashauri zetu ndani ya kata, vijiji watembeleeni wafugaji hao wa kuku badala ya kusubiri kukutana kwenye maonyesho kama haya,"alisema .

Alisema wafugaji hao wa kuku bado wanahitaji kupatiwa elimu ya mafunzo zaidi namna ya ufugaji ili kuboresha zaidi na kuwawezesha kupata masoko ya uhakika kwa wanunuzi na walaji wao.

**Hivyo kupitia kongamano hili nitumie nafasi hii pia niwaombe wataalam wetu mliopo kwenye halmashauri zetu ndani ya kata, vijiji watembeleeni wafugaji hao wa kuku badala ya kusubiri kukutana kwenye maonyesho kama haya**

# SUWASA yaanza mapambano kudhibiti upotevu wa maji

**Na Augusta Njoji,** SINGIDA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), imejipanga kukabiliana na upotevu wa maji wa asilimia 31 kwa kubadili miundombinu na mita za maji za zamani zinazosoma chini ya kiwango.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Sebastian Warioba, alisema upotevu wa maji unachangiwa na vitu mbalimbali mojawapo ni matumizi yasiyo sahihi au wizi wa maji na uchakavu wa miundombinu.

"Tunachofanya kuna maeneo tumefanya ukarabati, kubadilisha mita za zamani zinazosoma chini ya kiwango, mapema mwaka huu mamlaka hii imepata mita zaidi ya 20,000 za maji ambazo zinatumika kubadilisha na kuunganisha wateja, huku ikipewa mabomba ya zaidi ya Sh. milioni 300."

"Tunatarajia kupata mabomba mengine ya zaidi ya Sh.bilioni moja ili kubadilisha na kuunganisha kwa wateja ili kuondokana na upotevu wa maji," alisema.

**Tunatarajia kupata mabomba mengine ya zaidi ya Sh.bilioni moja ili kubadilisha na kuunganisha kwa wateja ili kuondokana na upotevu wa maji.**

Aidha, alisema katika kuimarisha upatikanaji wa maji Manispaa ya Singida inatekeleza kwa mradi wa maji wa miji 28 unaogharimu Sh.bilioni 45 ambao unatarajiwa kukamilika mwaka 2024.

Alisema mradi huo utaongeza upatikanaji wa maji na kuwafikia wateja kwa asilimia 90 kwenye Manispaa ya Singida.

Kadhalika, alisema kuna miradi mingine wanategemea kutekeleza kwa kupata fedha serikali kuu ili kuwafikia wananchi ambao hawajafikiwa na mtandao wa maji.

"Manispaa tuna kata 18 tumeshafikia kata 16 ambapo kuna baadhi hazijafikiwa kwa ukamilifu na zingine mbili hatujazifikia kabisa, tumewasilisha andiko Wizara ya Maji ili kupata fedha zaidi ya Sh.bilioni tatu," alisema.

Alibainisha kuwa mamlaka hiyo ina wateja wa maunganisho ya majisafi 18,000 na imewafikia kwa asilimia 78.

"Eneo tunalohudumia ni Manispaa ya Singida pamoja na miji mingine saba nje ya manispaa ambayo ni Buguno, Njia panda, Ikungi, Sepuka, Irisia, Puma na Makiungu ambapo tumewafikia wateja kwenye miji hiyo kwa asilimia 68," alisema.

Kuhusu uondoshaji wa majitaka, alisema manispaa hiyo haikuwa na huduma hiyo na kuanzia mwaka huu wameanza utekelezaji wa mradi wa uondoshaji majitaka ambapo wameanza na kujenga mabwawa eneo la Manga.

"Mabwawa haya yatakapokamilika mwishoni mwa mwaka 2024 tunategemea makazi ya wananchi yatakuwa salama kwa kuondosha majitaka na kupeleka kwenye mabwawa na maji hayo yatatibiwa na baadaye yataweza kutumika kwa manufaa ya kiuchumi ya wakazi wa hapa kama vile shughuli ya kilimo,"alisema.

Alitoa rai kwa wananchi kutoa taarifa pindi inapotokea hujuma kwenye maeneo ya miradi na miundombinu.




Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Deogratius Ndejembi, akipata maelezo kutoka kwa mwanakikundi wa chama cha wanawake 'Mathabita' Kiwanja cha Ndege jijini Dodoma, kilichopata mkopo wa asilimia 10 kwa ajili ya kujishughulisha na ukamuaji wa alizeti na usindikaji wa mazao ya nafaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahimizwa kutumia mbegu za TARI

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wamehimizwa kutumia mbegu za mtama zenye uwezo wa kukabiliana na gugu chawi ambazo zimefanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Akizungumza katika maonyesho ya nanenane Kanda ya Kati, Mtafiti na Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa kituo cha TARI Hombolo, Dk. Eliud Kongola, alisema mbegu hizo zina uwezo wa kukabiliana na gugu chawi ambalo limekuwa chanzo cha uharibifu wa zao hilo shambani.

Aidha, alisema mbegu hizo zitachangia kuongeza uzalishaji wa zao la mtama hapa nchini.

Alizitaja aina hizo za mbegu za mtama ni pamoja na wahi, Tari sogamwani, Tari soga Mtuu na Hakika ambazo zimefanyiwa utafiti.

"Katika maonyesho haya tumekuja na mbegu hizo pamoja na nyingine nyeupe zilizofanyiwa utafiti ambazo wakulima wanapaswa kwenda kuzitumia katika msimu wa kilimo huu ili kuongeza uzalishaji wa zao la mtama,"alisema.

Alisema mbegu hizo ni bora ambazo zitachangia kwa kiasi kikubwa mkulima kufanya kilimo chenye tija kitakachomsaidia kuingia katika soko la ushindani na kujikwamua kiuchumi.

Aliwaasa vijana wanaoingia katika kilimo kujikita kwenye kilimo cha mtama ili kuchangia kuongeza uzalishaji utakaokidhi mahitaji ya viwanda hapa nchini na nje ya nchi.

"Hivi sasa zao hili lina soko kubwa sana hapa ndani na nje, kutokana na kwamba linatumika katika matumizi mbalimbali ikiwemo kutengeneza vinywaji mbalimbali pamoja na utengenezaji wa masuala ya lishe,"alisema.

Naye, Ofisa Kilimo kutoka TARI Hombolo, Sabinus Kinunda, aliwataka wakulima kutumia kanuni za kilimo ambazo zitawasaidia kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawawezesha kuongeza uzalishaji.





# WMA yaagizwa kuhamasisha wakulima kujiunga vikundi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amewahimiza Wakala wa Vipimo (WMA), kuhamasisha wakulima kujiunga katika vikundi ama vyama vya ushirika (AMCOS) ambapo itakuwa rahisi kwa serikali kuwawezesha kuwa na mizani sahihi na iliyohakikiwa.

Amesema hilo likifanyika litawawezesha wakulima kuuza mazao kwa kuzingatia uzito sahihi unaotakiwa kisheria ambao ni uzito usiozidi kilo 100 na kuacha kufungasha na kusafirisha mazao kwa mtindo wa Lumbesa.

Kigahe aliyasema hayo alipotembelea banda la Wakala wa Vipimo katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nane Nane yanayofanyika kitaifa Jijini Mbeya kwenye Viwanja vya John Mwakangale.

Alisema WMA iendelee kuwasimamia wafanyabiashara kuhakikisha hawatumii vipimo batili kama ndoo, madebe na kangomba wakati wa uuzaji wa mazao yao kwani vipimo hivyo vinawapunja na kuwanufaisha wanunuzi.

Kadhalika, aliipongeza WMA kwa kuendelea kusimamia usahihi wa vipimo kwenye sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya kilimo.

**WMA inaendelea na usimamizi wa vipimo kwenye ufungashaji wa mazao ili kutokomeza ufungashaji wa mazao kwa mfumo wa lumbesa ambapo kaguzi mbalimbali zinafanyika ili kukabiliana na suala hilo.**

Naye Mkurugenzi wa Biashara wa WMA, Deogratias Maneno alimweleza Naibu Waziri, kuwa WMA ni wadau wakubwa kwenye maonyesho ya kilimo kwa kuwa inashiriki kwenye mnyororo mzima wa thamani tangu mkulima anapoanza uzalishaji wa mazao mpaka anapofika katika uzalishaji.

Pia, alisema WMA inaendelea na usimamizi wa vipimo kwenye ufungashaji wa mazao ili kutokomeza ufungashaji wa mazao kwa mfumo wa lumbesa ambapo kaguzi mbalimbali zinafanyika ili kukabiliana na suala hilo.

Alisema WMA inatumia nafasi ya ushiriki kwenye maonesho hayo ya wakulima kuwaelimisha wakulima.

Aliwataka wakulima wafuate sheria na taratibu ili waweze kuuza mazao kwa kutumia mizani na wafungashe na kusafirisha mazao kwa uzito usiozidi kilo 100.

Pia, alimweleza Naibu Waziri kuwa WMA inaendelea kuhimiza halmashauri mbalimbali kuanzisha vituo maalumu vya mauzo.

Alisema vituo hivyo vitasaidia wakulima kupeleka mazao yao na wanunuzi kununua katika vituo hivyo ambavyo vitakuwa na mizani sahihi iliyo hakikiwa na WMA ili kuhakikisha kunakuwa na biashara ya usawa bila mkulima kupunjika ili waweze kupata stahiki zao kulingana na kiasi sahihi cha mazao wanayouza.

Kadhalika, alimweleza Naibu Waziri kuwa WMA inaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi kwenye vyama mbalimbali vya ushirika vya msingi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima wa mazao ya kimkakati kama pamba, korosho, ufuta na kahawa ili waweze kutumia mizani wakati wa uuzaji wa mazao yao.

Mmoja ya wananchi aliyetembelea banda la WMA na kupata elimu kuhusu matumizi sahihi ya Vipimo, Lupakisyo Mahenge ambaye ni mkazi wa Mafinga alisema amejifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutambua namna sahihi za kuandika alama kwenye bidhaa zilizofungashwa.

Alisema amejifunza namna ya kutambua kama mzani umekaguliwa na WMA kupitia taarifa zinazojazwa kwenye vibandiko inayowekwa kwenye mizani ambayo inaonyesha mwaka na mwezi ambao kipimo kimekaguliwa.



Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, akizungumza alipotembelea banda la Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) kwenye maonyesho ya Nanenane jijini Mbeya. Wa tatu kulia ni Meneja Masoko na Mawasiliano wa TCAA, Yesaya Mwakifulefule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SBT, AgriCom zaingia makubaliano kukuza kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BENKI ya Stanbic Tanzania (SBT) kwa kushirikiana na kampuni ya zana za kilimo ya AgriCom Africa (AA) zimesaini hati ya makubaliano (MoU) yenye lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo kwa kuongeza matumizi ya zana bora na za kisasa.

Ushirikiano huo utawasaidia wananchi kunufaika na zana mbalimbali za kilimo zilizotengenezwa kwa teknolojia bora na ya kisasa kutoka AgriCom Africa kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kisasa katika sekta ya kilimo na kuongeza uzalishaji.

Aidha, wananchi pia wataweza kunufaika na mikopo ya kifedha katika sekta ya kilimo, biashara kwa zaidi ya silimia 80 kutoka benki hiyo, huku kukiwa na sharti la muda, ambapo wanaweza kulipa ndani ya miezi 60 (sawasawa na miaka mitano).

Zana hizo zitakazotolewa ni trekta, power tillers, uvunaji, post-harvesting machinery na zana nyingine muhimu katika shughuli za kilimo kwa wakulima.

Mpango huo wa ushirikiano unakwenda sawia na ajenda ya 10/30 ambayo inalenga kukuza sekta ya kilimo kwa zaidi ya asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 pamoja na kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa chakula nchini kitakachoweza kukidhi mahitaji ya ndani pamoja na kuuza nje ya nchi, hivyo kuongeza mapato kutoka kiasi cha Dola za kimarekani bilioni 1. mpaka Dola za marekani bilioni tano ifikapo mwaka 2030.

Akizungumza katika Viwanja vya Nanenane mkoani Mbeya, Mkuu wa Kitengo cha Mikopo ya Asseti na Vyombo vya Moto kutoka SBT, John Mosha alisema kuwa kupitia ushirikiano itasaidia wananchi husus ani wakulima kuwawezesha kununua zana za kilimo sambamba na kukopa vifaa na mashine mbalimbali za shambani ili kuongeza ufanisi na uzalishaji wenye tija.

# RC ahimiza wazazi kutunza kumbukumbu, historia ya taifa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema mbali na serikali kuwa na wajibu wa kutunza kumbukumbu na historia ya taifa kabla na baada ya uhuru, ipo haja ya wazazi kuweka utaratibu wa kuandaa taarifa ambazo huja kuwa kumbukumbu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Mtaka aliyasema hayo baada ya kutembelea banda la kumbukumbu za John Mwakangale kwenye Maonesho ya Nanenane ya Kitaifa yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.

"Mimi ninachoweza kusema maonyesho haya ni ya siku nyingi, lakini viwanja vya John Mwakangale ukimwambia mtu taja viwanja vya Nanenane unavyovifahamu, atakwambia viwanja vya John Mwakangale. Na pia mimi nimekutana na viongozi tofauti ambao hawamjui zaidi John Mwakangale alikuwa nani.

Alisema kwamba John Mwakangale ambaye ni miongoni mwa waasisi wa mwanzo waliokuwa bega kwa bega na Mwalimu Julius Nyerere ameacha kumbukumbu na heshima kubwa kwa taifa na mwenye uadilifu ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Hapa (katika banda) pana historia nzuri sana kwa sababu Mwakangale ni wale waasisi wa mwanzo ambao Mwalimu, alishirikiana nao kwenye harakati za uhuru na hata kwenye uanzilishi wa Chama cha TANU, na ni wale wabunge wa mwanzo ambao walikuja kushiriki kwenye serikali akawa waziri mdogo ambapo leo tunasema Naibu Waziri wa TAMISEMI," alibainisha Mtaka.

Kuhusu kumbukumbu kwenye banda hilo, Mtaka alisema ameshuhudia taswira za picha tofauti za harakati za ujenzi wa taifa pamoja na zilizowekwa kwenye maandishi.

"Ameshirikishwa kwenye mambo mengi, lakini kikubwa ni kwamba tuna Watanzania wengi sana wamenunua kitabu cha Nelson Mandela kiitwacho 'Long walk to freedom' na hawajui kuwa humu ndani ya kitabu hiki kimemnukuu John Mwakangale.

"Naamini watu wengi sana kwenye makabati ya vitabu walionyao nyumbani kwao hata maktaba za vitabu za Tanzania zenye kitabu hiki cha Mandela hawajui kuwa humu ndani kuna nukuu ya mtanzania," alisema Mtaka.

Alisema kumbukumbu ya John Mwakangale akinukuliwa kwenye kitabu hicho ambacho ni kikubwa kilichouzwa duniani katika tovuti na Amazon ni heshima kubwa kwa Watanzania.

"Mheshimiwa Kikwete (Jakaya) akiwa Waziri wa Madini alimtumia Mwakangale kadi ya kumtakia heri ya sikukuu na unaweza kuona huyu mtu alikuwa wa aina gani na baadae mheshimiwa Kikwete alikuja kuwa Rais, pia utaona hapa (katika banda) zipo kadi za sikukuu akipewa na Dk. Salim Ahmed Salim, Mwalimu Nyerere.

Alisema ipo haja ya viongozi na familia kuwafundisha watoto historia ya nchi yao, hususani kuhusu waasisi wa taifa ambao walijitoa kwa uzalendo kulipigania taifa kupata uhuru pamoja na kuandaa mazingira ya kimaendeleo ya nchi kufika sasa.

# Tanzania, Marekani wazindua kampeni ugawaji vyandarua

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Tanzania na Marekani wamezindua kampeni ya ugawaji vyandarua vyenye dawa kwenye kaya ikiwa ni jitihada za pamoja katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa kampeni hiyo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema: "Leo, tunasimama kwa pamoja katika dhamira yetu ya kupambana na ugonjwa wa malaria nchini Tanzania."

Alisema uzinduzi wa kampeni hiyo na ugawaji vyandarua vyenye dawa katika kaya za Mkoa wa Kagera na Tabora, Tanzania inatambua ushiriki wa Wamarekani pamoja na wadau wengine wa maendeleo.

Dk. Mollel alisema kupitia kampeni hiyo iitwayo 'Usingizi wa starehe' itasambaza vyandarua milioni 3.7 vyenye dawa katika kaya za Mkoa wa Kagera na Tabora.

"Kwa kubadilisha vyandarua vilivyochakaa na kuhakikisha upatikanaji wa vyandarua vipya, tunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya malaria na kulinda afya za jamii zetu." alisema.

Naye Mshauri Mkazi wa Masuala ya malaria kutoka USAID, Naomi Serbantez alisema: "Serikali ya Marekani inafurahi kuungana na wadau wetu wa malaria katika kuzindua kampeni hii ugawaji wa vyandarua vilivyotiwa dawa kwa jamii. Kwa kuhakikisha kuwa kaya zinapata vyandarua na vyandarua hivi vinatumiwa kwa usahihi ili kupunguza maambukizi ya malaria na kuwalinda watu walio katika mazingira hatarishi."

Alisema kupitia kampeni hiyo Marekani inasisitiza dhamira yake ya kuendelea kuisaidia Tanzania katika mapambano dhidi ya malaria na kuboresha afya na ustawi wa raia wake.

# Wahandisi wanawake nchini wakumbushwa kutumia fursa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, amewataka wahandisi wanawake kutumia fursa zilizotolewa na serikali kusajili kampuni na kujiajiri kupitia ukandarasi na ushauri elekezi ili kuchangia maendeleo ya nchi.

Alitoa rai hiyo wakati akifunga kongamano la nane la wahandisi wanawake Tanzania visiwani hapa, kuwataka wahandisi hao kuwafikia wanawake wengi zaidi hususani wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuoni ili kuongeza idadi ya wanawake wahandisi nchini.

**Maombi yapo hivyo wazazi na wanafunzi wanaohitaji kujiunga na chuo hicho ni vyema kuanza kufanya maombi ili kukuza zana ya sanyansi na teknolojia visiwani humo.**

Alisema Oktoba mwaka huu Zanzibar itafungua rasmi kampasi ya Chuo cha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mawasiliano cha India eneo la Bweleo ambacho kitaanza kutoa masomo ya data sayansi kiwango cha shahada ya kwanza.

Alisema maombi yapo hivyo wazazi na wanafunzi wanaohitaji kujiunga na chuo hicho ni vyema kuanza kufanya maombi ili kukuza zana ya sanyansi na teknolojia visiwani humo.

Aidha, alisema kongamano hilo kufanyika visiwani humo kumeihamasisha serikali, wanafunzi wa kike kusoma zaidi masomo ya sayansi ili kuwa na idadi kubwa ya wahandisi wanawake miaka ijayo.

Alisema serikali inakusudia kuwajengea uwezo wanafunzi wanawake wanaoendelea na masomo katika ngazi mbalimbali kupenda masomo ya sayansi kwa sababu mahitaji ya dunia kwa sasa ni masuala ya teknolojia.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhandisi Salha Muhammed Kassim ambaye ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) alisema hatua ya kongamano hilo kufanyika Zanzibar imeonesha hamasa ya kuwajali Wazanzibari ili kuzitambua fursa muhimu zilizopo hasa katika masomo ya sayansi.

Katika kongamano hilo lilowashirikisha washiriki zaidi ya 1,000 wakiwamo wahandisi kutoka ndani na nje ya nchi mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwamo nguvu ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za kihandisi ambapo ni mada muhimu katika kuimarisha maendeleo ya wanawake.

Katika kongamano hilo liliambatana na utoaji wa tunzo ya vinara kwa wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vikuu waliofanya vizuri katika kuonesha kazi za kisayansi na teknolojia ambapo mshindi wa mwanzo kwa upande wa shule tunzo hiyo ilichukuliwa na Shule ya Kisutu ya Dar es salaam na kwa chuo ilichukuliwa Chuo Kikuu cha Mbeya Sayansi na Teknolojia.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, akiwakabidhi kombe wanafunzi wa Chuo cha Mbeya Sayansi na Teknolojia kilichoibuka na ushindi wa kwanza katika maonyesho ya kazi za sayansi na teknolojia zilizofanyika katika kongamano la wahandisi wanawake Tanzania wakati akifunga kongamano hilo mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yajipanga 'kuteka' majimbo yote uchaguzi 2025

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimejipanga kuhakikisha majimbo yote ya uchaguzi yanabaki kuwa chini yao katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa CCM Jimbo la Chumbuni na Jimbo la Mpendae katika mwendelezo wa ziara yake ya kuimarisha chama visiwani humo.

Alisema CCM inaendelea na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 ambapo tayari miradi mbalimbali imeshakamilika na mingine inaendelea kujengwa ambacho ni kielelezo kikubwa cha wananchi kukikubali chama hicho hivyo ni vyema kuendelea kuchukua jitihada ili kukiimarisha na kuendelea kushika dola.

Hemed ambae pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema serikali inaendelea kutekeleza ilani ya chama kwa kujenga miradi mbalimbali ambayo kukamilika kwake itazalisha ajira ambazo vijana watanufaika kwa ajili ya kujipatia kipato na kupunguza ukali wa maisha.

Aidha, alisema kuwa Rais Dk. Mwinyi pamoja na wasaidizi wake wapo mstari wa mbele kuhakikisha wanawatumikia vyema wananchi wa Zanzibar na kuwasogezea huduma muhimu.

Pia aliupongeza uongozi wa Jimbo la Chumbuni kwa kuendelea kuongeza idadi ya wanachama wapya wa CCM hatua ambayo inaonesha wazi uwajibikaji wa viongozi wa jimbo hilo katika kuwatumikia wananchi wao.

Aliwasisitiza viongozi wa Chumbuni na Mpendae kuhakikisha kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ahadi zote walizoziahidi kwa wananchi wamezitekeleza ili kuwazidishia imani wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini kichama, Talib Ali alimpongeza Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kwa uamuzi wake wa kutembelea majimbo yote ya uchaguzi ambapo ziara yake hiyo itawakumbusha na kutilia mkazo utekelezaji wa ilani ya chama na utekelezaji wa ahadi walizoahidi kwa wananchi wakati wakiomba ridhaa.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Sufiani Khamis Ramadhan, alisema kuwa CCM Zanzibar kinaridhishwa na kasi ya utekelezaji wa ilani ya chama ya mwaka 2020-2025 chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Mjini, Idriss Kitwana Mustafa ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi alisema Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi itaendelea kusimamia amani na utulivu uliopo, ili serikali kutekeleza vyema majukumu yake ya kusimamia ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 378 LA 2023**

**ZAMZAM SHADADI**
**FIKIRI ISSA KOCHO {MUOMBAJI/WAOMBAJI}**
**DHIDI YA**

1. **AZIZA MALIKI**
2. **MAULID RAMADHAN**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **AZIZA MALIKI**
2. **MAULID RAMADHAN**

**POPOTE ULIPO/MLIPO:**
**ZAMZAM SHADADI** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nuymba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe **10/8/2023** saa tatu Asubuhi mbele ya **Mh. SILLAS**. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 4 Mwezi 8, 2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI


**NDAGALLA MAKOYE PETER**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA TOYOTA COROLLA NAMBA YA USAJILI T903 BBS. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**KAH/TR /RB/538/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA) 63**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA**
**KITUO CHA KARABAGAINE**
**SHAURI LA MADAI NO. 22/2023**
**MANSOUR IDRISA...............MDAI**
**DHIDI YA**
**ANGERO BAIKAINE & RUGEMALILA RUTATINA .........WADAIWA**

Angero Baikaine & Rugemalila Rutatina mnatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 10/08/2023 saa 08:30 asubuhi kuja kujibu madai mkiwa na mashahidi wenu.
Kwa kuwa ni siku ya kukata shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hili na kama hamtahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 28/07/2023.

**C. R. RICHARD**
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE**

## KUPOTEA KWA VYETI



**WILLY LAZARO** MLIGO anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: S3547/0110 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia HASANGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2013 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba: S0330/0689 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MBEYA SECONDARY SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: SIN/SIN/RB/303904/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ELISHA JAMES ISSANJA**
anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye usajili namba : T 659 AKW, T 746 ANT, T 463 ABP na T 346 DKY. Kwa yeyote atakaezionа atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**ARU/ARU/RB/257965/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **ANATH IBRAHIM ABDALLAH** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T 150 BGJ.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/264986/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au apige simu namba **0769-756081.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......44/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JUMA SELEMANI WA SAADANI - M/SONGO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ZAINABU NASSORO**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 10 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 04 mwezi 08 mwaka 2023

HAKIMU

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ufaransa yasitisha misaada Burkina Faso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

UFARANSA imetangaza rasmi kusitisha misaada ya maendeleo na bajeti iliyokuwa ikiitoa nchini Burkina Faso, tangazo hilo limetolewa siku chache baada ya nchi hiyo na Mali zitangaze kuunga mkono mapinduzi ya Niger.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa, hatua hiyo imekuja baada ya serikali ya kijeshi nchini Burkina Faso kusema kwamba ingechukulia uingiliaji wowote wa silaha dhidi ya viongozi wa mapinduzi katika nchi jirani ya Niger kama tangazo la vita.

Pia, ilielezwa kuwa hatua hiyo inakuja wakati Jumuiya ya Afrika Magharibi ECOWAS kwa viongozi wa mapinduzi ya kijeshi nchini Niger kuwataka kurejesha utulivu wa kikatiba na kumrejesha madarakani Rais aliyeondolewa Mohamed Bazoum.

Aidha, inaelezwa kuwa bado ECOWAS haijatoa tamko kuhusu hatua inayofuata ambayo ni pamoja na kuingilia kijeshi baada ya wito wake kupuuzwa.

Tume hiyo awali ilisema kuwa suala la hatua za kijeshi lingekuwa chaguo la mwisho iwapo mbinu zingine zote za kisiasa na kidiplomasia zitashindwa.

ANGA YAFUNGWA

Ilielezwa kuwa viongozi wa mapinduzi ya Niger wamefunga anga ya nchi hiyo kwa hofu ya kuvamiwa kijeshi, huku tovuti ya ufuatiliaji wa safari za ndege 'Flightradar24' ikionyesha kuwa kwa sasa hakuna ndege katika anga ya taifa hilo.

Awali ECOWAS ilionya kwamba inaweza kutumia nguvu ikiwa Rais Mohamed Bazoum hatarejeshwa madarakani ifikapo Jumapili ya juma lililopita.

Msemaji wa jeshi la serikali ya Niger alisema kuwa wanajeshi wa Niger wako tayari kuilinda nchi hiyo.

Bazoum alizuiliwa Julai 26, mwaka huu na Jenerali Abdourahmane Tchiani, kamanda wa walinzi wa rais, na baadaye kujitangaza kuma kiongozi mpya.

Mapinduzi hayo ya kijeshi yamelaaniwa kimataifa, ikiwa ni pamoja na Ufaransa na mataifa mengine ya Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na Umoja wa Mataifa (UN) na Marekani.

Baada ya mkutano wa dharura nchini Nigeria, wakuu wa jeshi la ECOWAS walisema kwamba wameandaa mpango wa kina wa uwezekano wa kutumia nguvu kurejesha utawala wa kiraia.

Kamishna wa ECOWAS anayeshughulikia masuala ya kisiasa, amani na usalama Abdel-Fatau Musa, alisisitiza kwamba wanataka diplomasia ifanye kazi, na wanataka ujumbe uwafikie bayana watawala wa Niger kwamba wanawapa kila fursa ya kubadili walichofanya.

"Masuala yote kuhusu hatua yoyote ya kuingilia kati yameshafanyiwa kazi, ikiwa ni pamoja na rasilimali zote zinazohitajika, namna gani na lini tutapeleka Jeshi," alisema Musa.

Ecowas ni jumuiya ya biashara ya kikanda ya nchi 15 za Afrika Magharibi, zikiwemo Nigeria, Senegal, Togo na Ghana.

**RFI, BBC**




Wafuasi wa kiongozi wa upinzani Ousmane Sonko, wakiandamana kwenye barabara za mji mkuu wa Senegal, wakipinga kukamatwa kwa kiongozi huyo. **PICHA: MTANDAO**

# Sonko alazwa baada ya kususia chakula jela

**DAKAR, Senegal**

RIPOTI ya chama cha kiongozi wa upinzani wa Senegal Ousmane Sonko, imesema kiongozi huyo ambaye amekuwa akisusia chakula wakati akiwa gerezani kama njia ya kulalamikia mashitaka ya jinai dhidi yake, amelazwa hospitalini licha ya sababu ya kulazwa kwake kutobainishwa.

Sonko, alipelekwa jela wiki iliyopita kabla ya kesi yake kusikilizwa, akituhumiwa kuitisha mapinduzi dhidi ya serikali ikiwa ni miongoni mwa mashitaka mengine.

Julai 30, Sonko kupitia ukurasa wake wa Twitter, alisema kwamba ataanza kususia chakula, na kwamba tangazo hilo lilikuja siku moja kabla ya Jaji wa mahakama ya Dakar kuamuru apelekwe jela.

Mashitaka ya karibuni dhidi ya Sonko yamekuja wiki chache baada jaji kumpata na hatia ya kuchochea vijana na kutoa hukumu ya miaka miwili jela, hatua iliyosababisha maandamano makali kote nchini Senegal.

Ilielezwa kuwa siku chache zilizopita, takriban watu wanne walikufa huku wengine kadhaa wakijeruhiwa kwenye maandamano mapya baada ya Sonko kupelekwa jela iliyoko nje kidogo ya mji mkuu wa Dakar.

Aidha, ilielezwa kuwa taarifa za hali ya afya ya Sonko zilikuja siku moja baada ya wakili wake Juan Branco, kukamatwa akiwa Mauritania na kisha kurejeshwa Senegal ambako amezuiliwa kwenye jela moja mjini Dakar.

Kwa mujibu wa wakili Robin Bindard. Sonko alishika nafasi ya tatu kwenye uchaguzi wa rais wa 2019, wakati akiwa na umaarufu mkubwa miongoni mwa vijana.

**VOA**

# Trump ataka kubadilishwa jaji anayesimamia kesi yake

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump amedai kuwa jaji wa serikali kuu alichaguliwa bila mpangilio kusimamia kesi inayomkabili akimtuhumu kwa njama ya kutaka kubadili kushindwa kwake katika uchaguzi wa 2020 na kwamba haitakuwa haki kwake huku akitaka abadilishwe.

Trump alisema jana kupitia mtandao wake wa Truth Social, kwamba kesi hiyo ni vyema ihamishwe kutoka Washington ambako kuna wakazi ambao kwa idadi kubwa hawakumpigia kura, ikielezwa kuwa jopo la mahakama linatarajiwa kuchaguliwa kutoka kwenye kundi la wapiga kura waliojiandikisha mjini humo.

Katika mtandao wake aliandika kuwa hakuna njia anaweza kuwa na kesi ya haki na hakimu aliyepewa aendeshe kesi, akimzungumzia Jaji wa Mahakama ya Wilaya Tanya Chutkan.

Wakili wa Trump John Lauro, alisema angependelea kesi ionyeshwe kwenye runinga akisisitiza kuwa hayo yalikuwa maoni yake binafsi

Pia ilielezwa kuwa wito unazidi kuongezeka kwa kesi za jinai za Trump kutangazwa moja kwa moja kwenye vyombo vya habari huku Marekani ikikabiliana na matarajio ya kumuona rais wa zamani na pengine baadaye akiwa kizimbani. Wanasheria na wanasiasa wanajitokeza kushinikiza kamera ziruhusiwe ndani ya chumba cha mahakama haswa wakati rais huyo wa zamani ambaye pia ni nyota wa TV za Reality anapokabiliana na mahakama kwa madai kwamba alijaribu kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa urais wa 2020.

Barua iliyosainiwa na mbunge wa California Adam Schiff na wenzake kadhaa wa Chama cha Democrat, ilieleza kuwa kwa kuzingatia hali ya kihistoria ya mashtaka yaliyowasilishwa katika kesi hizo ni vigumu kufikiria hali ya nguvu zaidi ya kesi zinazoonyeshwa kwenye televisheni.

"Ikiwa umma utapokea matokeo kamili itakuwa muhimu sana kwao kushuhudia moja kwa moja iwezekanavyo jinsi kesi zinavyoendeshwa nguvu ya ushahidi uliotolewa na uaminifu wa mashahidi," ilisema.

**VOA**

# JKU YAZIDI KUIWINDA VIKALI SINGIDA FG MICHUANO CAF

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya JKU ya visiwani Zanzibar wiki hii inatarajiwa kuelekea mkoani Morogoro kucheza michezo miwili ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa awali wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Singida Fountain Gate FC utakaopigwa Agosti 18, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana asubuhi baada ya kumaliza mazoezi kwenye Uwanja wa JKT Mbweni, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Ali, alisema Alhamisi wiki hii watacheza dhidi ya Dodoma Jiji FC na baada ya hapo, Jumapili watavaana na Geita Gold FC.

"Tutakwenda kucheza michezo miwili kwa ajili ya kukiimarisha kikosi changu kabla ya kuelekea kwenye michezo ya kimataifa dhidi ya Singida Fountain Gate," alisema Ali.


Kocha huyo alisema amebaini mapungufu kwenye safu yake ya ushambuliaji katika mchezo wa kirafiki walioucheza wiki iliyopita dhidi ya Yanga ambao walitoka sare ya kutokufungana.

Aliongeza kuwa tangu waanze kambi jijini Dar es Salaam, wachezaji wake wanaendelea vema kiafya isipokuwa mchezaji Gamba Iddy Matiko, ambaye aliumia mguu walipokutana na Yanga.

Alisema ameingalia Singida FG wakati walipocheza na timu ya AS Vita Club ya DR Congo na hajaona mchezaji hata mmoja atakayeweza kuwasumbua, kutoka na maandalizi wanayoendelea kuyafanya.

Timu hiyo ya Ligi Kuu Zanzibar, imeweka kambi yake JKT Mbweni kuanzia Agosti 3, mwaka huu ikijiandaa na mchezo wa kimataifa dhidi ya Singida Fountain Gate.

**MKONO WA MAMA...**




Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akisalimiana na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, wakati akitambulishwa wachezaji wa msimu mpya wa 2023, kwenye Tamasha la Simba Day, lililofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kuhitimishwa kwa timu hiyo kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, ambayo walishinda mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Mtibwa yasajili watano, yapandisha wawili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar imetangaza kusajili wachezaji wapya watano kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku ikipandisha wachezaji wawili vijana chini ya miaka 20.

Msemaji wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, amesema jana kuwa wanaamini wamesajili wachezaji ambao wataleta tija kwenye kikosi hicho hasa baada ya kutofanya vema kwa misimu kadhaa.

"Tulikaa chini na kuangalia aina gani ya usajili ambao tunatakiwa kufanya ili tusiwe tunaponea chupuchupu kushuka daraja," alisema Kifaru.

Taarifa iliyotolea na klabu hiyo ambayo ilitwaa Ubingwa wa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000, imewataja wachezaji waliosajiliwa kuwa ni Fredrick Magata kutoka Mbeya Kwanza, Abdul Hillary Hassan kutoka KMC, Juma Luzio ambaye amerejea tena kwenye kikosi hicho, Kassim Shaaban Haruna aliyekuwa akiichezea Polisi Tanzania, Abalkassim Suleiman na Kevin Nashon kutoka Singida Fountain Gate FC.

Mbali na wachezaji hao, Mtibwa Sugar pia imewapandisha wachezaji Omari Ally Marungu na Said Kazi ambao walikuwa kwenye kikosi cha timu hiyo kilichotwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Vijana chini ya miaka 20 hivi karibuni, michuano iliyofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. Marungu na Kazi ni kati ya wachezaji waliofunga mabao na kufanya vema kiasi cha kuingoza timu hiyo kuwa mabingwa.

Hata hivyo, Mtibwa ilimpoteza straika wake tegemezi ambaye alikuwa mfungaji bora wa ligi hiyo chini ya miaka 20, Athumani Masumbuko 'Makambo' ambaye baada ya kumalizika tu alinyakuliwa na Mashujaa FC.

## Dodoma Jiji yasaka tena viungo wanne

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji, imeamua kuingia tena sokoni kusaka viungo wanne kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake baada ya kugundua kuna baadhi ya mapungufu kwenye mechi zake za kirafiki.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Kassim Liogope, amesema baada ya kucheza mechi kadhaa za kirafiki wamegundua baadhi ya mapungufu kwenye kikosi, hivyo wanatakiwa kuyarekebisha haraka sana kabla ya kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hata msimu uliopita tulikuwa na tatizo kama hili, tunachofanya ni kuongeza watu eneo la kiungo na hao tutawapa majukumu, kazi yao itakuwa ni kutengeneza nafasi nyingi, hizi wiki mbili tulizokaa Iringa zimetunufaisha kwa sababu wachezaji wanaonekana kupokea vizuri mafunzo, tulicheza mechi za kirafiki ambazo zimetufanya tuone kuna baadhi ya mapungufu kwa hiyo sasa tunajitahidi kuyaziba ili kuhakikisha tukitoka hapa tupo kamili kwa mapambano,"alisema Liogope.

## TVF kuwafunda makocha wake

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Mpira wa Wavu Tanzania (TVF), kwa kushirikiana na Chama cha mchezo huo Mkoa wa Ruvuma (RUVA), kimeandaa kozi ya makocha itakayoanza Septemba Mosi hadi 9, mwaka huu mkoani humo.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Maendeleo Mikoani, Riziki Godwin, alisema lengo la kozi hiyo ni kupata makocha wazuri ambao watauendeleza mchezo huo zaidi.

"Tumeamua kuifanya kozi hiyo mkoani Ruvuma baada ya kupata maombi mengi kutoka kwa viongozi kutokana na kutokuridhishwa na mchezo huo mkoani Ruvuma," alisema Godwin.

Alisema mpaka sasa tayari makocha 22 wamethibitisha kushiriki na kudai mwisho wa uthibitisho ni Agosti 30, mwaka huu.

Alisema anaamini baada ya kumalizika kwa kozi hiyo watapata makocha wengi na kuwataka wadau wajitokeze kuchukua fomu ya ushiriki.

## ZISIKUPITE

### SALAH ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia, Al-Ittihad iko tayari kuipa Liverpool euro milioni 60 kwa ajili ya kumsajili Mohamed Salah na wako tayari pia kumlipa mshambuliaji huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 31, mshahara wa euro milioni 180 kwa mkataba wa miaka miwili. **(Al Riyadiah)**

### LUKAKU NAYE ASAKWA

KLABU za Ligi Kuu Saudi Arabia, Saudi Pro League, zinasaka majina makubwa zaidi kutoka Ligi Kuu England, akiwamo mchezaji wa Manchester City na Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 32 kwa kuelekeza nguvu kubwa mwaka ujao. **(Mirror)**

### BARCA YASAKA NYOTA

BARCELONA wamewasilisha ofa ya mkopo huko Manchester City kwa ajili ya wachezaji wawili wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 29 na Bernardo Silva (28) - na wako tayari kuwanunua moja kwa moja msimu ujao. **(Sport)**

### RAYA ANUKIA ARSENAL

JUHUDI za Arsenal kumpata mlinda mlango wa Brentford na Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 27, ziko katika hatua za mwisho. **(Fabrizio Romano)**

### MBAPPE AITAKA EPL

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kujiunga na Ligi Kuu ya England kwa mkopo wa msimu mmoja kabla ya kutimiza ndoto yake ya kuhamia Real Madrid. (Mirror)

### CAICEDO NA CHELSEA

CHELSEA wako tayari kuwasilisha ofa iliyoboreshwa ya kumnunua kiungo wa Brighton, Moises Caicedo baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21, kuachwa nje ya kikosi cha 'Seagulls' hao katika mechi yao ya kirafiki dhidi ya Rayo Vallecano. **(Telegraph)**

### ADARABIOYO APUUZA

MLINZI wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 25, amepuuzilia mbali mpango wa kuhamia Tottenham huku beki huyo wa England akitaka kujiunga na Monaco ya Ufaransa badala yake. **(Sun)**

### JORGINHO AWINDWA FENERBAHCE

KLABU ya Uturuki, Fenerbahce inavutiwa na kiungo wa Arsenal, Jorginho mwenye umri wa miaka 31, huku kukiwa na tetesi kwamba Muitaliano huyo hajatulia hapo Kaskazini mwa London. **(TRT)**

### SALANKE SASA AKATALIWA

KLABU ya Bournemouth imekataa ombi kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, West Ham kwa ajili ya mshambuliaji wao Dominic Solanke, 25. **(Daily Echo)**


### RAMSEY ATAJWA BURNLEY

KLABU ya Burnley imeongeza ofa yao hadi pauni milioni 12 kwa kiungo wa Aston Villa, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 20, na pia wanamwinda beki wa Manchester United, Alvaro Fernandez, 20. **(Mail)**

### ALVAREZ, WEST HAM BADO

DAU la West Ham la pauni milioni 25.9 kumnunua kiungo wa Ajax na Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 25, bado halijafikia thamani ya klabu hiyo ya Uholanzi. **(90 min)**

## DONDO… SOKA MA… AYA



# KEANE: FEDHA ILIYOLIPWA KWA RICE NI NYINGI MNO

Kwa hakika hana thamani ya zaidi ya pauni milioni 100, lakini ni mchezaji mzuri sana, hivyo...

**LONDON, England**

ROY Keane ameiambia Arsenal kuwa walilipa fedha nyingi sana kwa kiungo wa kati wa England, Declan Rice, walipotoa pauni milioni 105 kwa West Ham kwa ajili ya huduma yake.

Keane, ambaye alifanya kazi na Rice kama msaidizi wa Martin O'Neill wakati mchezaji huyo alipocheza mechi zake tatu za timu ya taifa ya wakubwa kwa Jamhuri ya Ireland, haamini kwamba anastahili bei hiyo.

Alipoulizwa kuhusu matarajio ya kiungo huyo hapo Kaskazini mwa London baada ya mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City Jumapili ambapo alicheza mechi yake ya kwanza ya ushindani, Keane aliiambia ITVI: "Ni wazi atazungukwa na wachezaji bora, mahitaji tofauti.

"Ikiwa atacheza juu zaidi juu ya uwanja, nadhani ana ubora huo katika kuongeza mabao zaidi. Ni wazi ana nguvu hiyo ya kimwili, anaweza kuingia kwenye sanduku.

"Ni wazi wamelipa fedha nyingi sana kwake. Kwa hakika hana thamani ya zaidi ya pauni milioni 100, lakini ni mchezaji mzuri sana.

"Tutajua mwaka ujao au miwili jinsi Declan ni mzuri. Yeye hujidhihirisha kila wiki, yeye ni mvulana mkubwa mwenye nguvu - tena, unazungumza juu ya hali hiyo ya mwili, walikosa hiyo katika mwezi uliopita au mbili (za msimu uliopita).

"Amepata ubora wa hali ya juu kiasi cha kuona pasi na kufunga mabao tisa, 10? Tutajua hivi karibuni."

Uhamisho wa Rice kwenda kwenye Uwanja wa Emirates mwezi uliopita baada ya kuwasaidia West Ham kushinda Ligi ya Europa Conference uliweka rekodi mpya ya uhamisho kwa England.

Mchezaji huyo mzaliwa wa London, ambaye babu na babaye wanatoka Cork, ameichezea mara 43 England, lakini alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa kwa Ireland, akicheza mechi za kirafiki dhidi ya Uturuki, Ufaransa na Marekani mwaka 2018 kabla ya kubadili na kuitumikia England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 667,

MECHI KALI

BARCELONA
VERSUS
TOTTENHAM

1 | 1.72
X | 3.71
2 | 4.02

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA AKUNWA NA KIWANGO CHA ARSENAL NGAO YA JAMII

**LONDON, England**

MIKEL Arteta hakuweza kuficha furaha yake baada ya Arsenal kuishinda Manchester City na kutwaa Ngao ya Jamii, Jumapili.

'Washikabunduki' hao walianza kufungwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu England kwa bao la Cole Palmer dakika ya 77.

Lakini Arsenal walifanikiwa kusawazisha mambo kwenye Uwanja wa Wembley dakika ya 101 kwa bao la Leandro Trossard aliyetokea benchi.

Bao la Mbelgiji huyo, ambalo lilisababisha mchezo huo kwenda kwa mikwaju ya penalti, ambapo Arsenal waliibuka washindi kwa 4-1 na kufanikiwa kutwaa taji la 17 la Ngao ya Jamii.

Kevin De Bruyne na Rodri wote walikosa penalti, huku Fabio Vieira akifunga ya kwanza.

Kuhusu ushindi huo muhimu Arteta alisema: "Tunajisikia vizuri.

"Nadhani ni bora zaidi kushinda kombe kwenye uwanja wa Wembley dhidi ya timu bora zaidi duniani kwa njia ambayo tulifanya."

Arteta pia alimsifia kipa Aaron Ramsdale, ambaye aliokoa kwa ustadi penalti ya Rodri.

Mhispania huyo aliongeza: "Yeye (Ramsdale) alikuwa mzuri. Tunafanya mazoezi ya penalti mara nyingi kwa makusudi kabla ya msimu ili kuwa tayari kwa hili endapo itawezekana.

"Tulipitia masikitiko dhidi ya Manchester United, kwa mfano, na hatukuzuia lolote kati ya hayo.

"Huo ulikuwa mwelekeo wa kujifunza ambao wakati mwingine unahitajika ili kupata matokeo sahihi mwishoni. Nadhani alikuwa mzuri sana."

# Ramos kumbadili Mbappe PSG

**PARIS, Ufaransa**

WAKATI Mshambuliaji, Kylian Mbappe akisumbua vichwa vya mabosi wa PSG hatma yake ikiwa haijulikani, taarifa zinadai mabosi wa klabu hiyo wapo kwenye mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Benfica, Goncalo Ramos mwenye umri wa maika 22, katika dirisha hili ili akaongeze nguvu eneo la ushambuliaji.

Ramos ambaye msimu uliopita alifunga mabao 27, alionesha kiwango bora kwenye Fainali za Kombe la Dunia zilizofanyika Qatar akiwa na timu yake ya Taifa ya Ureno na kuwavutia vigogo vya barani Ulaya.




Hata hivyo, changamoło kubwa inatajwa kufanikisha dili hilo ni kiasi cha fedha ambacho Benfica inakihitaji, ambapo inadaiwa klabu hiyo inataka pauni milioni 80 ili kumwachia mshambuliaji huyo ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2025.

Kuna uwezekano mkubwa PSG ikamsajili mshambuliaji huyo hata kabla ya kumpiga bei Mbappe kwani hata kama staa huyo atabaki ndani ya viunga vya Princes Park huenda asitumike kwenye kikosi.

Mbappe alibaki Paris wakati timu yake iliposafiri kwenda barani Asia kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, wakati hayo yakiendelea PSG ikatangaza kumuuza staa huyo wa Kimataifa wa Ufaransa.

Katika dirisha lililopita la majira ya baridi vigogo mbalimbali pamoja na Manchester United vilionesha nia ya kutaka kumsajili Ramos.

HABARI MICHEZO

,592,120

# ROBERTINHO AFUNGUKA, ONANA ASEMA BADO

**Na Saada Akida**

BAADA ya kucheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa ya kirafika msimu huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, Kocha Mkuu wa Klabu ya Simba, Robertinho Oliveira, amesema wachezaji wake wapo tayari, lakini hawezi kufanya mabadiliko ya haraka ya kikosi chake huku kiungo mshambuliaji mpya, Willy Essomba Onana naye akisema "hapa ni mwanzo tu".

Simba ilicheza mechi hiyo katika Tamasha la Simba Day, ikitokea kambini Uturuki ambapo ilicheza michezo mingine mitatu ya kirafiki kabla ya kurejea nchini.

Akizungumzia kikosi chake, Robertinho alisema kundi la wachezaji wa kwanza wako tayari kwa mapambano ya mashindano yaliyoko mbele yao, lakini bado anahitaji kupata muda zaidi wa kuupata muunganiko wa timu nzima ili kuendeleza rekodi ya matokeo mazuri katika mashindano yaliopo mbele yake.

Alisema bado anahitaji kupata muda wa kutosha ili kuweza kupata muunganiko wa timu yote kutokana na mashindano makubwa yaliyopo mbele yao, lakini akisisitiza kwa sasa anaweza kupata matokeo dhidi ya timu yoyote.

"Kambi yetu imetusaidia kwa sababu tumeweza kuimarisha eneo la kiungo, nilikuwa na makundi mawili ya kuwasoma wachezaji, ukiangalia kama Ngoma amecheza vizuri japo haikuwa rahisi kutengeneza uelewano kwa timu mpya, lakini baada ya mchezo nimeongea na Kibu (Denis), Saido (Ntibanzokiza) na Chama (Clatous) kwa ushirikiano bora waliofanya na kusababisha kupata matokeo mazuri.

"Sasa tunajiandaa na Super League (African Football League), kwa sababu timu ya kwanza ipo tayari, ila siwezi kubadili timu ya kwanza haraka kwani bado nahitaji muda zaidi wa kuweza kuijenga timu ya pili na kupata muunganiko wa timu nzima, utasaidia kuonyesha soka ambalo nalitaka lichezwe hapa kwa lengo la kupata matokeo mazuri katika michezo ambayo tutacheza," alisema Robertinho.

Kwa upande wa Kocha wa Power Dynamo, Mwenya Chipepo, alisema nafasi waliyoipata kucheza na Simba kwao kilikuwa kipimo sahihi kuelekea katika michuano iliyopo mbele yao huku akiwapongeza Simba kwa kuweza kuonesha kiwango kizuri kwenye mchezo huo.

Wakati huo huo, Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Willy Essomba Onana, amesema mashabiki wa timu hiyo watulie waone mipango yake ndani ya timu hiyo kwa kuwa lengo lake ni kuona anafunga mabao katika kila mchezo atakaocheza kwani bado hajafikia kwenye ubora wake.

Alisema amefurahi kuwa miongoni mwa wachezaji waliofanikiwa kufunga katika mchezo wa kwanza ndani ya timu hiyo huku akisisitiza kuwa bado amejipanga kuweza kufunga sana ili kufikia malengo ya timu hiyo katika michuano ya kimataifa.

"Nashukuru Mungu kwa kuweza kuniwezesha kuwa mmoja kati ya wachezaji waliofunga bao katika mchezo mkubwa mbele ya mashabiki wengi ambao wamejitokeza kutupa sapoti, hili ni jambo kubwa kwangu, lakini bado kuna kazi kubwa iliyopo mbele yetu.

"Nadhani hapa ni mwanzo kwa sababu nataka kuona nafunga sana katika kila mchezo ambao nitacheza kwa lengo la kuisaidia timu katika mashindano ambayo tunaenda kushiriki, kikubwa ni kwa mashabiki kuendelea kutuombea na kutupa sapoti ya kutosha kwa kuweza kufika katika mechi zetu," alisema Onana.

# CAF yaiondoa Simba Ligi Kuu mwezi mmoja

INATOKA UK. 24

unaenda kuweka taswira ya kipekee baada ya timu hizo zote kufanya usajili mzuri wa kuvutia.

Mechi mbili kubwa zingine ni kati ya Yanga dhidi ya Azam FC utakaopigwa Oktoba 25 saa 12:00 jioni, huku Simba dhidi ya Azam FC wakipangwa kukutana Novemba 28, mwaka huu, saa 11:00 jioni mechi zote mbili zikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi mbili zitakazofungua pazia la ligi hiyo hapo Agosti 15, ni Ihefu FC dhidi ya Geita Gold FC utakaopigwa katika Uwanja wa Highland Estate, uliopo Mbarali mkoani Mbeya, ukitarajiwa kuchezwa saa 10:00 alasiri na mwingine ukiwa kati ya Namungo FC itakayowakaribisha JKT Tanzania katika dimba la Majaliwa, lililopo Ruangwa mkoani Lindi.

Agosti 16, mwaka huu Dodoma jiji FC itakuwa mwenyeji wa Coastal Union, wakati huo Mashujaa FC wakiwakaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Agosti 17 kutakuwa na michezo miwili kati ya Azam FC dhidi ya Kitayosce FC mchezo utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Mtibwa Sugar dhidi ya Simba Uwanja wa Manungu mkoani Morogoro.

Singida Fountain Gate FC itawakaribisha Tanzania Prisons katika dimba la Liti Singida, mechi itakayochezwa Agosti 22 na kesho yake Yanga ikiialika KMC FC katika Uwanja wa Azam Complex.

Aidha, Kasongo alisema katika ratiba hiyo wamezingatia mashindano yote ya kimataifa kwa ngazi ya klabu na timu za taifa.

Alisema walifanya kazi kubwa sana kupanga ratiba hiyo kwa kuepuka viporo vingi kwa kuzingatia michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa klabu mbili za Simba na Yanga pamoja na Kombe la Shirikisho Afrika ambazo Azam FC na Singida Fountain Gate FC zitaiwakilisha nchini.

"Tumeangalia pia mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo Tanzania Bara hutoa timu tano zinazoenda visiwani kwenye mashindabo hayo, Kombe la Shirikisho la FA, Michuano ya AFCON 2023 ambapo Tanzania tutacheza Septemba mwaka huu, michuano ya CHAN 2024 inayotarajiwa kufanyika Guinea.

Michuano mingine ni ya kufuzu AFCON 2025 na Kombe la Dunia mwaka 2026 itakayofanyika Marekani, Canada na Mexico pia ratiba imeangalia mashindano hayo," alisema Kisongo.

## Yanga yaionya Azam FC Ngao

INATOKA UK. 24

nye Kombe la FA bao 1-0, sisi tunaiandaa timu yetu, kama hawatokuwa bora au kujiandaa vizuri tutawapa adhabu ile ile ambayo waliipata kwenye mechi ya mwisho, akili yetu ni kuijadili furaha yetu na siyo maumivu ya watu wengine," alisema Kamwe.

Alisema wachezaji wa Yanga wapo Tanga wakiwa wanajua kuwa wametumwa taji hilo na wachama na mashabiki, si vinginevyo.

"Majembe yanaendelea kunolewa vizuri tu, wanachama na mashabiki wa Yanga watakachokitaka Tanga ni kurejea na Ngao ya Jamii hakuna stori nyingine," alisema Ofisa Habari huyo.

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/08/23 | 19:00 | VPS Vaasa vs Seinajoen JK | 2.91 | 3.06 | 2.27 |
| 02. 09/08/23 | 19:00 | Hodd vs Sandnes Ulf | 2.42 | 3.24 | 2.58 |
| 03. 09/08/23 | 20:00 | AEK Larnaca vs Maccabi Tel Aviv | 2.81 | 3.16 | 2.46 |
| 04. 09/08/23 | 20:30 | Chippa Utd vs TS Galaxy FC | 2.68 | 2.98 | 2.62 |
| 05. 09/08/23 | 20:30 | Polokwane City vs Stellenbosch | 3.00 | 2.95 | 2.23 |
| 06. 09/08/23 | 21:30 | Slovan Bratislava vs Maccabi Haifa | 3.13 | 3.13 | 2.22 |
| 07. 09/08/23 | 21:30 | Austria Klagenfurt vs Wolfsberger AC | 2.43 | 3.33 | 2.51 |
| 08. 09/08/23 | 22:45 | Benfica vs Porto | 2.21 | 3.17 | 3.02 |
| 09. 10/08/23 | 18:00 | FC Struga Trim Lum vs Swift Hesperange | 2.39 | 3.36 | 2.76 |
| 10. 10/08/23 | 19:00 | Omonia Nicosia vs Midtjylland | 2.59 | 3.24 | 2.59 |
| 11. 10/08/23 | 20:00 | Dila Gori vs Apoel Nicosia | 2.96 | 3.16 | 2.35 |
| 12. 10/08/23 | 20:00 | Valmiera Fk/Bjss vs Partizani Tirana | 3.06 | 3.26 | 2.24 |
| 13. 10/08/23 | 21:30 | Hibernian vs FC Luzern | 2.66 | 3.36 | 2.46 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 08/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4546 | France W vs Morocco W | 1.15 | 6.51 | 13.21 |
| 15:00 | 5532 | Persis Solo vs Persib Bandung | 2.67 | 3.33 | 2.30 |
| 16:00 | 4177 | Kelantan United FC vs Terengganu | 6.85 | 4.84 | 1.32 |
| 16:00 | 5680 | Kedah vs Pahang FA | 2.18 | 3.40 | 2.70 |
| 16:15 | 5112 | Ural Yekaterinburg vs Rostov | 2.33 | 3.20 | 2.79 |
| 16:30 | 1891 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs WIT Georgia | 2.74 | 3.35 | 2.29 |
| 17:00 | 1177 | Astana vs Ludogorets Razgrad | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 18:00 | 1007 | Znicz Pruszkow vs KS Gornik Polkowice | 1.47 | 3.92 | 6.11 |
| 18:00 | 2321 | SK Bela vs MSK Fomat Martin | 6.08 | 5.47 | 1.33 |
| 18:00 | 2494 | Dinamo-2 Tbilisi vs Loko Tbilisi | 1.57 | 4.36 | 4.26 |
| 18:00 | 4725 | Richards Bay FC vs Golden Arrows | 2.39 | 2.88 | 3.09 |
| 18:00 | 4928 | BFC Daugavpils vs Rigas Futbola Skola | 14.33 | 6.34 | 1.15 |
| 18:30 | 2506 | Rubin Kazan vs Lokomotiv Moscow | 2.60 | 3.21 | 2.48 |
| 20:00 | 3498 | Helsingborg vs Orgryte IS | 2.21 | 3.40 | 3.09 |
| 20:30 | 2266 | Orlando Pirates vs Bloemfontein Celtic | 1.43 | 4.11 | 6.79 |
| 20:45 | 5947 | Spartak Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.53 | 3.98 | 5.10 |
| 21:00 | 1920 | Rakow Czestochowa vs Aris Limassol | 1.89 | 3.31 | 3.86 |
| 21:00 | 2611 | Copenhagen vs Sparta Prague | 2.08 | 3.36 | 3.21 |
| 21:00 | 4287 | Huddersfield vs Middlesbrough | 3.03 | 3.38 | 2.18 |
| 21:00 | 5041 | Barcelona vs Tottenham | 1.72 | 3.71 | 4.02 |
| 21:30 | 2273 | PSV Eindhoven vs Sturm Graz | 1.39 | 4.65 | 6.33 |
| 21:30 | 2743 | Mansfield vs Grimsby | 1.82 | 3.59 | 3.88 |
| 21:30 | 4357 | Swansea vs Northampton | 1.55 | 4.07 | 5.16 |
| 21:30 | 4821 | Peterborough vs Swindon Town | 1.55 | 4.18 | 4.97 |
| 21:30 | 5751 | Newport vs Charlton | 2.99 | 3.39 | 2.19 |
| 21:45 | 1816 | Notts County vs Lincoln | 1.99 | 3.49 | 3.39 |
| 21:45 | 1939 | Stevenage vs Watford | 3.24 | 3.39 | 2.08 |
| 21:45 | 2087 | Derby vs Blackpool | 1.91 | 3.58 | 3.53 |
| 21:45 | 2554 | Accrington vs Bradford City | 2.64 | 3.29 | 2.49 |
| 21:45 | 2765 | AEK Athens vs Dinamo Zagreb | 2.17 | 3.23 | 3.13 |
| 21:45 | 2791 | Hull City vs Doncaster | 1.51 | 4.19 | 5.38 |
| 21:45 | 2821 | Stoke City vs West Bromwich | 2.26 | 3.14 | 3.09 |
| 21:45 | 3183 | Preston vs Salford City | 1.72 | 3.84 | 4.09 |
| 21:45 | 3329 | Plymouth vs Leyton Orient | 1.66 | 3.84 | 4.48 |
| 21:45 | 3448 | Blackburn vs Walsall | 1.50 | 4.30 | 5.40 |
| 21:45 | 3505 | Barnsley vs Tranmere | 1.62 | 3.98 | 4.58 |
| 21:45 | 4084 | Millwall vs Reading | 1.51 | 3.94 | 5.98 |
| 21:45 | 4347 | Sunderland vs Crewe | 1.36 | 4.79 | 7.18 |
| 21:45 | 4390 | Forest Green vs Portsmouth | 3.44 | 3.49 | 1.97 |
| 21:45 | 4731 | Harrogate vs Carlisle | 2.94 | 3.34 | 2.24 |
| 21:45 | 4737 | Rotherham vs Morecambe | 1.49 | 4.29 | 5.59 |
| 21:45 | 5144 | Sheffield Wed vs Stockport | 1.70 | 3.74 | 4.39 |
| 21:45 | 5358 | Gillingham vs Southampton | 4.68 | 3.93 | 1.62 |
| 21:45 | 5366 | Bolton vs Barrow | 1.64 | 3.88 | 4.58 |
| 21:45 | 5528 | Port Vale vs Fleetwood Town | 2.32 | 3.32 | 2.83 |
| 21:45 | 5646 | KI Klaksvik vs Molde | 4.66 | 3.72 | 1.65 |
| 21:45 | 5692 | Cheltenham vs Birmingham | 3.04 | 3.39 | 2.17 |
| 22:00 | 1641 | Wrexham vs Wigan | 1.91 | 3.49 | 3.64 |
| 22:00 | 3321 | Olimpija Ljubljana vs Galatasaray | 4.63 | 3.77 | 1.64 |
| 22:00 | 4587 | Sporting Braga vs Backa Topola | 1.19 | 6.13 | 11.87 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Agosti 8, 2023

Nipashe




## Keane: Fedha iliyolipwa kwa Rice ni nyingi mno

UKURASA 21

## RATIBA TOP 3 LIGI KUU BARA



Robertinho

**MTIBWA SUGAR VS SIMBA**
AGOSTI 17 (MANUNGU COMPLEX)-MOROGORO

**SIMBA VS DODOMA JIJI**
AGOSTI 20 (UHURU STADIUM)- DAR

**PRISONS VS SIMBA**
OKTOBA 3 (SOKOINE STADIUM)-MBEYA

**SIMBA VS COASTAL UNION-TBA**
(UHURU STADIUM) DAR ES SALAAM

**SINGIDA FG VS SIMBA-TBA**
(LITI STADIUM) SINGIDA



Gamondi

**YANGA VS KMC**
AGOSTI 23 (AZAM COMPLEX) DAR ES SALAAM

**YANGA VS JKT TANZANIA**
AGOSTI 29 (AZAM COMPLEX) DAR ES SALAAM

**YANGA VS NAMUNGO-TBA**
(AZAM COMPLEX) DAR ES SALAAM

**IHEFU VS YANGA**
OKTOBA 4 (HIGHLAND ESTATES) - MBEYA

**GEITA GOLD VS YANGA**
OKTOBA 22 (NYANKUMBU STADIUM) GEITA



Youssoupha Dabo

**AZAM VS KITAYOSCE**
AGOSTI 16 (AZAM COMPLEX) DAR ES SALAAM

**AZAM VS PRISONS**
AGOSTI 28 (AZAM COMPLEX) DAR ES SALAAM

**AZAM VS SINGIDA FOUNTAIN GATE-TBA**
(AZAM COMPLEX) - DAR ES SALAAM

**DODOMA JIJI VS AZAM**
OKTOBA 3 (JAMHURI STADIUM) DODOMA

**COASTAL UNION VS AZAM**
OKTOBA 21 (MKWAKWANI STADIUM) TANGA

NB: TBA NI MECHI AMBAZO HAZIJAPANGIWA TAREHE

# CAF YAIONDOA SIMBA LIGI KUU MWEZI MMOJA

●●●Kuvaana na Yanga Novemba 8, kipenga chapulizwa rasmi huku...

**Na Saada Akida**

WAKATI Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ikitangaza ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2023/24, itaanza rasmi Agosti 15 na kutamatika Mei 29, mwakani, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limelitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuiondoa Klabu ya Simba kwenye ratiba hiyo kwa mwezi mmoja kuanza Oktoba 20 hadi Novemba 21, mwaka huu.

Hatua hiyo, imekuja kutokana na kibarua kigumu ambacho Klabu ya Simba itakuwa nacho ndani ya mwezi huo kwenye michauano mipya ya CAF, African Football League (Super League), inayoshirikisha timu nane bora barani Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa kutangaza ratiba ya Ligi Kuu msimu wa 2023/24, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema wamefanya mawasiliano na wanaosimamia mashindano ya Super League (CAF), ambao wametaka kuiondoa Simba katika ratiba ya mechi za Ligi Kuu katika kipindi cha Oktoba 20 hadi Novemba 21, mwaka huu ili kumpa nafasi ya kujiandaa na michuano hiyo.

"Baada ya kukutana na waaandaji hao walitueleza kuwa ratiba ya michuano hiyo bado haijatoka na inatarajiawa kutoka kati ya wiki ya pili ya Septemba, hivyo wametusisitizia kuiondoa Simba katika tarehe hizo kwa kuwapa nafasi ya kufanya maandalizi mazuri.

"Tunatambua mashindano hayo yanayoshirikisha timu nane kubwa barani Afrika na Tanzania ni wenyeji wa mashindano hayo huku Simba ikiwakilisha taifa letu, hali hiyo tumeamua kupanga ratiba kuwa rafiki kwa kuzipa nafasi wawakilishi wetu katika michuano ya kimataifa kufanya vizuri," alisema Kasongo na kuongeza:

"Tumekutana na mazingira magumu ya kupanga ratiba kwa sababu ya mashindano mengi yaliyopo hapa nchini ikiwamo kwa timu zetu nne zinazoenda kushiriki (michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika)."

Kuhusu ratiba ya Ligi Kuu Bara, Kasongo alisema siku ya ufunguzi Agosti 15, zitachezwa mechi mbili huku miamba ya soka nchini Simba na Yanga ikipangwa kukutana katika raundi ya nane, Novemba 8, mwaka huu.

Mchezo huo ambao Simba atakuwa mwenyeji huku ukitarajiwa kupigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 11:00 jioni,

UKURASA. 23

## Yanga yaionya Azam FC Ngao

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeionya Azam FC ikiiambia kama haijajiandaa vizuri na kuwa bora msimu huu, basi itarajie kukutana na kipigo kikali kesho kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema wanaitaka Azam FC iwe imejiandaa kisawasawa kwani wanachama na mashabiki wa Yanga wamewaambia hawataki kitu kingine kwenye Makao Makuu ya Klabu hiyo, Jangwani zaidi ya kurejea na Ngao ya Jamii.

Tayari timu zote zimeshatua jijini Tanga kwa ajili ya michuano hiyo ambayo msimu huu Inachezwa kwa mfumo wa mtoano, ikizishirikisha mechi nne, badala ya Bingwa wa Tanzania Bara na wa Kombe la FA kama ilivyokuwa huko nyuma.

"Hatuna muda wa kujali au kuangalia hasira za Azam FC kwa sababu eti tuliwafunga kwe

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >